SUPA JACKPOT
TZS. 1,159,574,731
KWA TZS. 1000 TU!
SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SportPesa.CO.TZ
PIGA *150*87#

Jumamosi Oktoba 7, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

# Nipashe

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0581456
www.ippmedia.com
www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US

**Ajali** ya mabasi ilivyoua watu 7 na kujeruhi 22

UKURASA 2



**Matinyi** aanika mambo muhimu ya kuanza nayo

UKURASA 3



**Wanafunzi** walazwa madai ya kula viazi vyenye sumu

UKURASA 4

# Rugambwa: Nina mzigo mkubwa

• **ATAKA** Watanzania wamwombee, amtaja Pengo ukardinali.. *Uk. 3*



Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango akifurahia jambo na Mwadhama Kardinali Protase Rugambwa, baada ya kumpokea alipowasili katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere, jijini Dar es Salaam jana, akitokea Vatican. **PICHA: OMR**

## YALIYOMO

UKURASA WA 4

### WAMLILIA CHONGOLO KULIWA NA MAMBA



WANANCHI wa Kata ya Ugala, Halmashauri ya Nsimbo mkoani Katavi, wamemweleza Katibu Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Daniel Chongolo, adha wanayoipata pindi wanapokwenda kutafuta maji Mto Ulanga ikiwamo...

## Mganga matatani madai vifo vya mapacha

UKURASA 2

## Madudu yaibuliwa upimaji ardhi, PM ataka wahusika wawajibishwe

UK. 2

**MICHEZO** YANGA KUMALIZA HASIRA KWA GEITA UK.24

**MAONI** UK.6



Balozi wa Sweden nchini, Charlo Ozaki Macias (katikati), akikata utepe kufungua ofisi mpya ya Umoja wa Klabu za Waandishi wa Habari Tanzania (UTPC), eneo la Kilimani, jijini Dodoma juzi. Wengine ni Mkurungenzi Msaidizi Idara ya Habari Maelezo, Zamaradi Kawawa (kulia), Rais wa UTPC, Deogratius Nsokolo (wa pili kulia), Mkurungenzi wa UTPC, Kenneth Simbaya (kushoto) na Ofisa Ubalozi huo, Holger Tausch. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Madudu yaibuliwa upimaji ardhi, PM ataka wahusika wawajibishwe

**Na Beatrice Shayo**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, ameibua madudu katika upimaji ardhi huku baadhi ya maofisa wa serikali wakimiliki kampuni zinazofanya kazi hiyo.

Kutokana na hali hiyo, ameagiza kampuni zilizopewa kazi za upimaji wa viwanja jijini Dodoma na kushindwa kukamilisha kazi hiyo, zichukuliwe hatua kali za kisheria.

Pia ameagiza kukamatwa na kuchunguzwa na vyombo vya dola vibarua Justin Albert, Freddy Mathias, Elias na Magige ambao wanatembea na nyaraka za serikali na kuuza viwanja kwa niaba ya maofisa wa jiji.

Majaliwa aliagiza hayo jana katika kikao alichokiitisha ofisini kwake, Mlimwa jijini Dodoma, cha viongozi wa majiji ya Dar es Salaam, Mwanza, Arusha, Mbeya, Tanga na Dodoma, kujadili migogoro ya ardhi iliyokithiri kwenye majiji hayo na kutafuta suluhisho.

"Mkurugenzi alikuwa na kampuni mbili, Mhasibu wake ana kampuni yake wanazitumia kupima maeneo, kwa hiyo ni miradi yao," alibainisha.

Majaliwa aliagiza vibarua hao kuzirejesha nyaraka za serikali wanazozitumia vibaya kwa kuendelea kuuza viwanja maeneo ya jiji ya ukanda wa kijani, Mkonze, Ndachi, Chinyika, Ng'ong'ona na Mkalama. "Hawa ni vibarua lakini wana ramani na wanavijua viwanja vyote. Wanachofanya ni kufanya mauzo halafu wanapeleka kwa watu wao pale jiji na hati zinatoka. Kwa hiyo, watafutwe na wanyang'anywe zile nyaraka ili wasiendelee kuuza viwanja," aliagiza.

Kuhusu kampuni hizo, Majaliwa alisema: "Moja kati ya hatua hizo ni kuzi 'blacklist' (kuzifutia usajili) kwa sababu kampuni hizo hizo tutumie kampuni ambazo zina uaminifu badala ya kutumia ambazo zinatuzalishia migogoro."

Alisema wanatambua kampuni nyingi Dodoma ni za watumishi wenyewe kama ilivyoelezwa kwenye ripoti.

Majaliwa aliwaagiza wakuu wa mikoa wahakikishe kamishna msaidizi wa mkoa, maofisa mipango miji wa majiji, halmashauri na manispaa hawana sababu ya kuchukua watumishi wa muda kufanya kazi ya upimaji bali wafanye wao ili kuepusha mianya ya rushwa.

## Ajali ya mabasi ilivyoua watu 7

**Na Said Hamdani,** LINDI

WATU saba wamefariki dunia na wengine 22 kujeruhiwa baada ya mabasi ya Saibaba na Baharia kugongana uso kwa uso katika kijiji cha Kiwawa, Kilwa mkoani hapa.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Lindi, Kamishna Msaidizi (ACP) Pili Mande, alisema ajali hiyo ilitokea jana saa 8:00 mchana kwa kuhusisha basi namba T 604 DJJ aina ya Scania mali ya Kampuni ya Saibaba, lililokuwa likiendeshwa na Lucas John likitokea Nachingwea kwenda Dar es Salaam.

Alitaja basi lingine ni aina ya TATA lenye namba T 217 DXG la Kampuni Baharia, lililokuwa likiendeshwa na Omar Abdallah, likitokea Dar es Salaam kwenda Tandahimba mkoani Mtwara.

Kamanda Mande alisema madereva hao ni miongoni mwa watu saba waliofariki dunia katika ajali hiyo. Lucas (59) ni mkazi wa jijini Arusha na Omari (57) ni mkazi wa Dar es Salaam.

Mande alisema chanzo cha ajali hiyo ni dereva wa Saibaba kulipita lori lililokuwa mbele yake kwenye kona kisha kugongana uso kwa uso na basi la Baharia, hivyo kusababisha vifo hivyo.

Alisema majeruhi wote wamepelekwa katika Hospitali ya Kinyonga wilayani Kilwa kwa matibabu huku miili ikihifadhiwa hospitalini hapo.

Mganga Mfawidhi wa Hospitali hiyo, Dk. Lusajo Mwakajoka, alisema wamepokea miili saba kati yao wanaume ni watano na wanawake wawili na majeruhi 22, wanaume wakiwa 11 na wanawake 11.

Alisema majeruhi hao wameumia maeneo mbalimbali ya miili yao na wawili wakiwa na majeraha kichwani.

Dk. Mwakajoka alisema baadhi ya majeruhi walikuwa na hali mbaya, hivyo walikuwa wanawaandaa kuwasafirisha kwenda Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH).

# Mganga matatani madai vifo vya mabinti wawili mapacha

**Na Vitus Audax,** BARIADI

MKUU wa Wilaya ya Bariadi, Simon Simalenga, ameliagiza jeshi la polisi mkoani Simiyu kumsaka na kumkamata mganga wa tiba asilia, Masunga Tumolo, mkazi wa kijiji cha Byuna kwa madai ya kusabibisha vifo vya mabinti wawili mapacha wenye umri wa miaka 17.

Mganga huyo anadaiwa kusababisha vifo vya mabinti hao waliohitimu kidato cha nne mwaka jana katika Shule ya Sekondari Mkororo baada ya kuwapaka dawa kwenye matiti yao kwa lengo la kuongeza ukubwa wa maumbile hayo ili waozeshwe na mama yao.

Mabinti hao, wakazi kijiji cha Bubale kilichoko Kata ya Nkololo wilayani hapa, walipoteza maisha baada ya kukosa nguvu na kujihisi maumivu kwa siku mbili baada ya kupakwa dawa hizo walipopelekwa na mama yao mzazi.

Akizungumza juzi katika eneo la tukio, Simalenga aliliagiza jeshi hilo kuhakikisha mganga huyo anakamatwa na kuchukuliwa hatua za sheria kwa kusababisha vifo vya mabinti hao.

"Kwa kuwa tayari mke wake amepatikana, aendelee kushikiliwa wakati huo mkiendelea kumtafuta mme wake (mganga wa tiba asilia) popote alipo lazima apatikane. Haya ni mauaji kama mauaji mengine lazima achukuliwe taratibu za kisheria," aliagiza.

Simalenga pia aliliagiza jeshi la polisi kuwakamata wote waliohusika katika tukio hilo wakiwamo wazazi wa mapacha hao huku akisisitiza jamii kuacha tabia za kuwaozesha watoto katika umri mdogo na kuwaacha waendelee na masomo.

"Mama aliona anachelewa na anataka apokee mahari na watoto hawabadiliki akaamua kuwapeleka kwa mganga wa kienyeji wakapakwe dawa ili kifua kibadilike haraka. Matokeo yake wote wamepoteza maisha kutokana na dawa waliyopewa na mganga huyo. Tumepoteza watoto wawili kwa tamaa ya mahari," alisema.

Wanafamilia wa mama huyo walisema aliwadanganya kuwa anawapeleka watoto hao hospitali lakini baada ya kufika huko alibadili uamuzi na kuwapeleka kwa mganga wa kienyeji ambaye aliwapaka dawa hizo na kuanza kupoteza nguvu na kulegea.

Majirani wa mganga huyo walisema mabinti hao walifikishwa kwa mganga huyo kwa ajili ya kuoga dawa ya kuotesha matiti huku wakikemea tabia hizo ambazo zimekuwa zikifanyika mara kwa mara.

"Tunaomba serikali ifanye ufuatiliaji juu ya tiba zinazotolewa na waganga hawa maana kuna wengine hatujui labda wamewahi kufa na kufichwa hivyo wafuatiliwe na kuchukuliwa hatua pale wanapokiuka utaratibu wa kisheria," alisema Mwanaidi Hamisi.

Mganga Mfawidhi wa Kituo cha Afya cha Byuna, Dk. Degratius Mtaki, alithibitisha vifo vya mapacha hao na kueleza kuwa awali alipokea mwili wa Doto kisha kumpokea Kulwa akiwa mahututi na baada ya muda alifariki dunia.

"Doto Yohana (17) ndiye alipokewa kwanza tulimfanyia uchunguzi na kubaini kuwa tayari amefariki dunia. Pia tulimpokea Kulwa Yohana (17) ambaye alikuwa mahututi tukafanya vipimo kisha naye akafariki dunia. Tulibaini kuwa wametapika kwa muda mrefu na kupoteza nguvu," alisema Dk. Mtaki.



Mwonekano wa njia ya chini ya waenda kwa miguu iliyoko kwenye barabara ya Lumumba eneo la Mwanga Sokoni, mkoani Kigoma jana, iliyojengwa kwa fedha za Mfuko wa Barabara. **PICHA: NEEMA EMMANUEL**

# Rugambwa: Nina mzigo mkubwa, niombeeni

**Na Beatrice Shayo**

ASKOFU Mkuu Mwandamizi wa Kanisa Katoliki Jimbo Kuu la Tabora, Mwadhama Protase Kardinali Rugambwa, amesema ana mzigo mkubwa wa kutimiza wajibu aliopewa huku akitaka waumini na Watanzania wamwombee.

Amesema kuteuliwa katika daraja hilo ni kutimia kwa kauli ya Askofu Mkuu Mstaafu wa Jimbo Kuu la Dar es Salaam, Mwadhama Polycarp Kardinali Pengo, aliyemtabiria siku moja kuwa, akirudi Tanzania atakuwa na nafasi kubwa bila kuitaja.

Akizungumza jana jijini Dar es Salaam muda mfupi baada kuwasili akitokea Vatican nchini Italia, Kardinali Rugambwa alisema anamshukuru Mwenyezi Mungu kwa kurejea salama na kuomba aombewe ili kuyatenda yaliyo mema kulingana na vazi hilo alilovalishwa ambalo ni zuri.

Mapokezi ya Kardinali Rugambwa katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere (JNIA), yaliongozwa na Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango.

Septemba 30, mwaka huu, Kiongozi wa Kanisa Katoliki Duniani, Papa Francis, aliwapandisha maaskofu wakuu 21 kuwa makardinali, akiwamo Rugambwa.

Kardinali Rugambwa alisema anashukuru Kardinali Pengo aliyemwambia mwaka 2012 kuwa wito aliopewa wa kuwa Balozi wa Papa akiufanya vizuri anaweza kurudi nyumbani akiwa na wadhifa mkubwa ambao wakati huo hakuutaja.

"Utabiri huu naona umetimia. Nimerudi nyumbani nikiwa Kardinali. Ninakushukuru sana (Kardinali Pengo) kwa ushauri mbalimbali ulionisaidia katika majukumu yangu nikiwa Vatican.

"Kuvaa dera ni rahisi ila kazi kulishika. Leo hii nina wadhifa wa Kardinali mabegani mwangu. Jukumu langu kubwa kuyafanyia kazi hayo majukumu mapya niliyo nayo. Ni majukumu mazito, peke yangu siyawezi nahitaji sala zenu,"aliomba.

Kardinali Pengo alisema anashukuru kwa kupata msaidizi wa kazi hizo za kanisa na kuwaomba Watanzania kumwombea.

Alimkumbusha Kardinali Rugambwa kuwa nyakati fulani alimtabiria kuwa akifanya vizuri huenda akarudi nyumbani na madaraka makubwa.

Makamu wa Rais, Dk. Mpango, alisema Kardinali Rugambwa ameiletea sifa Tanzania na dhamira ya serikali ni kushirikiana na viongozi wa dini kuendeleza amani na kuimarisha umoja wa kitaifa.

Alisema serikali itaendelea kushirikiana na kanisa hilo na madhehebu mengine kuleta maendeleo na kuhimiza umoja, amani na utulivu.

Dk. Mpango alisema uteuzi wa Kardinali Rugambwa ni kielelezo na ushuhuda wa ukweli kwamba Tanzania ni nchi ya amani na imekuwa na bahati ya kuwa na Kardinali ambaye ni wa tatu baada ya Laurean Kardinali Rugambwa na Kardinali Pengo.

"Rais Samia Suluhu Hassan yuko nje ya nchi kikazi na anatarajia kwenda India kwa ziara ya kikazi. Kwa niaba yake, serikali na Watanzaia karibu nyumbani. Tumefurahi tumepata baraka kama ulivyosema. Ni baraka kubwa kwa nchi yetu," alisema Dk. Mpango.

Alisema kwa mara ya tatu wamejaliwa kupata Kardinali na wanaamini kwa Tanzania wanaposema wana amani ni kutokana na mambo mazuri kama hayo ambayo Mungu anaendelea kuyakirimia.

Kwa niaba ya serikali, alisema wanampongeza na wanachozidi kuomba ni amani ya taifa walimfuatilia alivyokuwa Vatican nchini Italia aliendelea kusisitiza amani na umoja kwa Watanzania.

"Katika nafasi hii mpya sijajua wataendelea kukuweka Tabora, sijui watakuweka wapi. Lakini tunaamini kabisa utaendelea kuwa chumvi ya amani, umoja na upendo kwa Watanzania," alisema.

Aidha, alisema Rais Samia atakaporejea nchini atafanya utaratibu wa kumkaribisha nyumbani kwa kuwa ni mkuu wa nchi.

Mwenyekiti wa Umoja wa Wanawake Wakatoliki Tanzania (WAWATA), Evelyne Ntenga, alisema wanaendelea kumuombea kwa Mungu ili kazi aliyoipokea aifanye kwa uadilifu.

Alitaka wanawake watenge muda na kukaa na watoto ili kuwasaidia kile ambacho Mungu amekiweka ndani yao ili wawe na maadili mema.

# Matinyi ataja mambo ya kuanza nayo

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

MKURUGENZI wa Idara ya Habari -MAELEZO na Msemaji Mkuu wa Serikali, Mobhare Matinyi, amesema moja ya mambo ambayo atayapa kipaumbele katika uongozi wake ni tatizo la vyombo vya habari kukosa ushirikiano kutoka kwa maofisa wa serikali.

Matinyi alibainisha hayo jana jijini hapa wakati akizungumza na waandishi wa habari mara baada ya kukabidhiwa ofisi na mtangulizi wake, Gerson Msigwa.

Alisema tatizo la maofisa wa serikali kutotoa ushirikiano kwa vyombo vya habari linachangia kwa kiasi kikubwa wananchi kushindwa kufahamu kazi kubwa ambayo inafanywa na serikali.

"Hili lazima nilifanyie kazi ili kufahamu shida iko wapi kama ni serikali au vyombo vya habari kwani kuna miradi mikubwa ambayo serikali inatekeleza sasa lakini wananchi hawaifahamu.

"Kuna ujenzi wa barabara, madarasa, miradi mikubwa ya afya na mingine mingi lakini wananchi hawafahamu," alisema Matinyi ambaye aliteuliwa na Rais Samia Suluhu Hassan hivi karibuni kushika wadhifa huo.

Matinyi ambaye alikuwa Mkuu wa Wilaya ya Temeke kabla ya uteuzi huo, alisema idara yake itaanzisha utaratibu wa kutoa elimu kwa maofisa wa serikali kuhusu umuhimu wa kutoa taarifa kwa vyombo vya habari badala ya kuendelea kuogopa na kujificha.

"Tunajua wengi wao ni waoga kutoa taarifa na sababu ninadhani mnazijua. Unakuta mwandishi aanakuja anaambiwa mkuu hayupo, kumbe yuko ndani na wengi wao wamekuwa wakifanya hivi," alisema.

Matinyi alisema kupitia mafunzo hayo, watafahamishwa namna ya kuzungumza na vyombo vya habari ili kutoa taarifa zitakazofahamisha ili wananchi wajue nini serikali inafanya.

Pia aliwataka wanahabari wanapopewa taarifa na viongozi wazingatie usahihi wake wanapoziandika ili kuondoa mkanganyiko ambao unaweza kujitokeza.

"Habari siku zote ni usahihi. Mtu ukibadilisha hata nukta tu umeharibu maana nzima, hivyo lazima wanahabari tuwe makini katika suala zima la usahihi, kwani mnaweza kusababisha viongozi hawa waviogope vyombo vya habari na kuikosesha jamii taarifa muhimu," alikumbusha. Matinyi alimshukuru Rais Samia kwa kumwamini na kumteua katika nafasi hiyo na kuahidi kuendeleza mazuri yote yaliyofanywa na mtangulizi wake.

"Nitahakikisha ninaendeleza yale mazuri yote ambayo ameyafanya mwenzangu (Msigwa) na kuendelea kuisemea serikali yetu ili wananchi wajue nini serikali yetu inafanya"alisisitiza.

Msigwa ambaye kwa sasa ni Katibu Mkuu Wizara ya Sanaa, Utamaduni na Michezo, akimkabidhi ofisi hiyo, alimpongeza Matinyi kwa kuteuliwa na kuahidi kumpa ushirikiano wakati wote.

www.nbc.co.tz

TAARIFA KWA UMMA

KUHAMA KWA TAWI LA NBC KARIAKOO

Tunapenda kuwataarifu wateja wetu kuwa kuanzia Jumatatu tarehe 9 Oktoba 2023 tawi letu la NBC Kariakoo litahamia Mkunguni Street, Nyumba no. 22.

Tunapenda kuwahakikishia wateja wetu wote kuwa hakutakuwa na usumbufu wala upungufu wowote katika utoaji wa huduma zetu wakati wa kuhama na baada ya kuhama. Huduma zote tunazozitoa katika tawi la NBC Kariakoo zitaendelea kutolewa kwenye eneo jipya.

NBC inayonia na kusudi la kuwahudumia wateja wetu kwa ufanisi zaidi.

Imetolewa na Uongozi wa Benki ya Taifa ya Biashara (NBC)

NBC
Benki ya Taifa ya Biashara
Daima Karibu Nawe.

# Wanafunzi 11 wanusurika kifo madai ya kula viazi vyenye sumu

**Na Francis Godwin,** IRINGA

WANAFUNZI 11 wa Shule ya Msingi Gangilonga, Mufindi mkoani hapa, wamelazwa katika Hospitali ya Wilaya ya Mufindi baada ya kula viazi aina ya kachori vinavyodaiwa kuwekwa sumu ya panya na mtoto mwenzao.

Mtoto huyo wa darasa la tano shuleni hapo, baada ya kusoma kuwa ukiweka hamira katika kachori, watakaokula matumbo yataumuka, aliporudi nyumbani alichukua sumu ya panya akidhani ni hamira na kuweka katika viazi.

Mwenyekiti wa Mtaa wa Gangilonga iliyoko shule hiyo, Samson Mwanselelo, alisema jambo hilo limewatia hofu na kuzua taharuki na hawakulitarajia wala halijawahi kutokea kwenye mtaa wake.

Mwanselelo alisema tukio hilo limetokea kutokana na watoto kunyang'anyana vyakula wanavyotoka navyo nyumbani.

Alisema mmoja wa wanafunzi hao alisikia kuwa ukiweka hamira kwenye kachori basi watakaokula watauмuka matumbo.

"Hili tukio limesababishwa na mwanafunzi wa darasa la tano ambaye alipata somo kuwa akiweka hamira kwenye kachori basi wale watakaokula wataugua matumbo, sasa huyo akaweka akidhani ni hamira kumbe ilikuwa sumu ya panya," alisema.

Mmoja wa wazazi, Monica Lubida, alisema alipata taarifa ya tukio hilo na anashukuru Mungu mtoto wake ni mzima na kutoa wito kwa serikali kupiga marufuku watu wote wanaouza vyakula karibu na shule.

Lubida alisema watu hao wanauza vyakula shuleni kama maandazi na kachori wanaweza kuwa moja ya chanzo cha watoto kulishwa vyakula ambavyo vina madhara kwao.

Alibainisha kuwa shule zimeweka utaratibu wa watoto kula shuleni, hivyo ni vyema utaratibu huo ukafuatwa na kila mzazi akawajibika kulipia chakula kwa ajili mtoto wake na si nje ya shule ili kuepuka madhara.

"Wanaouza vyakula shuleni wazuiwe kwa maana huwezi jua kila mmoja anapikia kwake. Sasa hawa leo wamekula kachori zenye sumu, utashangaa kesho (watoto) wamekula maandazi yenye sumu, hivyo ni vyema wote wakazuiwa kuuza shuleni," alisema.

Kubida alitoa wito kwa wazazi kushiriki kuchangia chakula cha wanafunzi kama walivyokubaliana kwenye vikao vya wazazi, ili kuepuka na tabia ya wanafunzi kubeba vyakula kutoka majumbani kuja navyo shule.

Akizungumzia tukio hilo, Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Wilaya ya Mufindi, Dk. Victor Msafiri, alisema wamepokea watoto 11 na kati ya hao saba walipatiwa matibabu na kuruhusiwa na wanne wanaendelea na matibabu.

"Ni kweli tulipokea jana (juzi) watoto 11 kutoka Shule ya Msingi Gangilonga walisadikiwa kula chakula chenye sumu.

Tumewapatia matibabu na saba hali zao ziko vizuri tumewaruhusu. Wanne bado wamelazwa wanaendelea na matibabu na kesho (leo) tunatarajia kuwaruhusu hali zao zikiimarika," alisema.

Dk. Msafiri alitoa wito kwa wazazi kuwalea vizuri watoto wao na kuweka mbali dawa au sumu za kuulia wadudu waharibifu kama mende na panya ili zisiwadhuru watoto.

Pia aliwataka wazazi na walezi kutoa elimu kwa watoto kuhusu vitu vya hatari kama hivyo vya sumu ili wasiguse.




Mwakilishi wa Bakhresa Group, Hussein Suphiane (katikati), akichangia mada kuhusu "Kuelewa mfumo wa kodi wa Tanzania kwa Maendeleo Endelevu ya Sekta ya Viwanda", wakati wa kongamano la wenye viwanda lililoandaliwa na Shirikisho la wenye Viwanda Tanzania (CTI), jijini Dar es Salaam jana. Wengine ni Mwakilishi wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Stephen Magige (kushoto) na Nguvu Kamando kutoka Vodacom Tanzania. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wananchi wamlilia Chongolo kuliwa na mamba

**Na Neema Hussein,** NSIMBO

WANANCHI wa Kata ya Ugala, Halmashauri ya Nsimbo mkoani Katavi, wamemweleza Katibu Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Daniel Chongolo, adha wanayoipata pindi wanapokwenda kutafuta maji Mto Ulanga ikiwamo baadhi yao kuliwa na mamba.

Waliyasema hayo jana baada ya Chongolo kutembelea na kukagua mradi wa maji Katambike ambao unadaiwa kucheleлewa kutokana na mkandarasi aliyekuwa akiutekeleza, kufariki dunia katika ajali ya ndege iliyotokea wilayani Bukoba.

Kutokana na kilio hicho, Chongolo aliahidi mabadiliko katika mradi huo baada ya siku 21, kwa kuwa wamepewa dhamana ya kusimamia na kuleta matokeo ya kubadilisha na kuboresha huduma kwa wananchi.

"Dhamana hii ni kubwa na inatutaka tubebe dhamira ya dhati ya kutekeleza hayo ndani ya mioyo yetu. Hatuwezi kuacha Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan anahangaika, anakesha kutafuta fedha zinashuka huku kwa ajili ya kutatua changamoto zenu,' alisema.

Akisoma taarifa ya utekelezaji wa mradi huo, Meneja wa Wakala wa Maji Vijijini (RUWASA) Wilaya ya Mpanda, Christian Mpena, alisema kukamilika kwa miradi miwili ya maji ukiwamo wa Katambike, kutarahisisha upatikanaji wa huduma kutoka asilimia 40.8 mpaka 80.

Mpena alisema mradi huo kwa sasa umefikia asilimia 25 na utakapokamilika, utawanufaisha zaidi ya wananchi 12,000 na taasisi za kiserikali zikiwamo Shule ya Msingi Ugala, kituo cha afya na taasisi za dini.

Alisema mradi huo pia utapunguza vifo vya wananchi waliokuwa wanafuata maji Mto Ugala na kuliwa na mamba pamoja na kupunguza magonjwa yatokanayo na ukosefu wa maji safi na salama.

Ujenzi wa mradi huo, alisema ulianza kutekelezwa Juni 21, 2022 na ulitarajiwa kukamilika Desemba, mwaka huu. Mkandarasi ameongezewa muda mpaka Oktoba 30, mwaka huu, ili kuukamilisha. Mradi huo unatarajiwa kugharimu zaidi ya Sh. milioni 700.

# Watoto wauawa kikatili madai ya kulipiza kisasi

**Na Neema Hussein,** MPANDA

WATOTO wawili wameuawa kikatili kwa madai ya kulipiza kisasi, baada ya mwanamume aliyemtaka kimapenzi mwalimu aliyekuwa akiishi na watoto hao kumkataa.

Waliouawa ni Mariam Mtemvu (13) ambaye alikuwa dada wa kazi katika familia hiyo na Ester Zuberi mwenye umri wa miaka miwili katika familia hiyo.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Katavi, Kaster Ngonyani, akizungumza na waandishi wa habari juzi, alisema tukio hilo lilitokea katika kijiji cha Kabatini, Wilaya ya Tanganyika.

"Chanzo cha mauaji haya ni mapenzi. Mmoja kati ya watuhumiwa hao (wanaoshikiliwa) alimpenda mwalimu anayefahamika kama Rose kimapenzi lakini mwalimu huyo alimkataa," alisema.

Kamanda Ngonyani alisema kutokana na mwanamume huyo kukataliwa, aliamua kukodi mtu na kumlipa Sh. 400,000 ili kumuua mwalimu huyo kwa madai kuwa amekula fedha zake nyingi bila mafanikio.

"Mtuhumiwa alipokea zile fedha baada ya kufika nyumbani kwa mwalimu hakumkuta, akaamua kuingia ndani kuiba chochote cha thamani, baada ya msaidizi wa ndani (dada wa kazi) kupiga kelele, akaamua kumkata panga yeye na mtoto," alisema.

Alisema kutokana na tukio hilo ambalo chanzo chake kinatajwa kuwa ni wivu wa mapenzi, tayari watu wanne wanashikiliwa na Jeshi la Polisi kwa madai ya kuhusika na mauaji hayo.

Kamanda Ngonyani alisema watoto hao waliuawa kwa kukatwa na kitu chenye ncha kali maeneo mbalimbali ya miili yao.

Alisema familia iliyopatwa na tatizo hilo ni ya mwalimu aliyetambulika kwa jina la Rose ambaye anafundisha katika Shule ya Msingi Kabatini.

Alisema wakati tukio hilo likitokea Mwalimu huyo alikuwa shuleni na aliporudi nyumbani ndipo alipokuta mauaji hayo yametokea.

Kamanda Ngonyani alisema baada ya kupata taarifa za mauaji hayo, wamewakamata watuhumiwa wanne waliohusika na tukio hilo.

Alisema bado wanaendelea na mahojiano baada ya upelelezi kukamilika watawafikisha mahakamani kujibu tuhuma zinazo wakabili.

Katika tukio lingine, Kamanda Ngonyani alisema polisi inawashikilia watu wanne wanaodaiwa kuhusika na unyang'anyi wa kutumia nguvu kwa kumpiga mtu mmoja na kumnyang'anya zaidi ya Sh. milioni moja alizokuwa nazo.

Alisema watuhumiwa hao walimpiga mtu huyo na kitu kizito kichwani na sasa amelazwa hospitalini kwa matibabu.

## HABARI KITAIFA

# Naibu Waziri ambana mkandarasi malipo ya wafanyakazi na vibarua

**Na Faustine Feliciane**

NAIBU Waziri wa Uchukuzi, David Kihenzile, ameagiza taasisi zilizo chini ya wizara hiyo kuwasimamia makandarasi kwenye miradi ya ujenzi na kuwalipa kwa wakati wafanyakazi wao, wakiwamo vibarua.

Kihenzile alitoa agizo hilo jana jijini Dar es Salaam wakati akikagua mradi wa ujenzi wa jengo la Kituo Kikuu cha Utabiri na Ofisi ya Kanda ya Mashariki ya Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA).

Alisema kumekuwa na malalamiko mengi ya wafanyakazi wazawa wanaofanya kazi kwenye miradi ya ujenzi kunyanyaswa na kutolipwa stahili zao kwa wakati jambo ambalo serikali inalipinga.

"Kuanzia sasa, taasisi ambazo zipo chini ya wizara hii, wawasimamie makandarasi na wahimize kuwalipa fedha kwa wakati wafanyakazi wao kwa sababu serikali inawalipa kwa wakati makandarasi hao," alisema Kihenzile.

Alisema kamwe hawatakubali kuona Watanzania wenye kipato cha chini wanaonewa kupata haki yao wakati serikali imekuwa ikilipa fedha za makandarasi kwa wakati.

"Najua katika mradi huu wa jengo la TMA mambo kama hayo hakuna, nawapongeza sana, lakini ninawaomba makubaliano ya ujenzi huu yaheshimiwe na mradi ukamilike kwa wakati," aliagiza.

Alitaka ujenzi wa jengo hilo la ghorofa tano uende sawa na thamani ya fedha zinazotolewa.

Mhandisi Mshauri wa ujenzi huo, Dk. Johnson Malisa, alisema ujenzi huo wenye thamani ya Sh. bilioni 9.9 umepangwa kukamilika Julai 24, 2024.

"Tumeanza ujenzi mwezi Januari, mwaka huu, na mpaka sasa tumefikia asilimia 35, ghorofa tatu zitakuwa ofisi na mambo mengine na ghorofa mbili za juu zitakuwa kwa ajili ya kusimika mitambo ya hali ya hewa," alisema Dk. Malisa. Mwenyekiti wa Bodi ya ya Mamlaka hiyo, Dk. Burhan Nyenzi, alisema kukamilika kwa jengo hilo kutatoa fursa kwa Tanzania kuwa na kituo kikubwa cha masuala ya utabiri na ufuatiliaji wa matukio ya majanga Afrika.

"Hapa kutakuwa na ofisi, lakini kutakuwa kituo cha watu kuja kujifunza kutoka ndani na nje ya nchi, Tanzania ni nchi iliyopewa jukumu la kuratibu masuala mbalimbali ya hali ya hewa kikanda, hivyo kutakuwa na watu wengi kutoka nchi mbalimbali za Afrika watakaokuja hapa kujifunza na kufanya kazi. Jengo hili ni muhimu," alisema.

Dk. Nyenzi alisema bodi anayoiongoza itaendelea kusimamia utendaji kazi wa menejimenti ya Mamlaka hiyo ili iendelee kuwa juu na mfano wa kuigwa.

# Simbachawene ataja mbinu za kukabili uhalifu kimtandao

**Na Mary Mosha,** MOSHI

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, George Simbachawene, amesema serikali imejizatiti kukabiliana na uhalifu wa kimtandao.

Hatua hiyo ni baada ya kuimarisha wataalamu katika Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) ambao watakuwa na uwezo wa kukatisha mifumo ya rushwa kabla haijatekelezeka.

Akifunga jana mafunzo ya uchunguzi wa awali kwa waajiriwa wapya wa taasisi hiyo, yaliyofanyika katika Shule ya Polisi Moshi, mkoani hapa, alisema serikali katika ngazi mbalimbali inaendesha miradi mingi ikiwamo ya afya, elimu na maji ambayo imekuwa na wastani wa Sh. bilioni sita hadi 200. Simbachawene alisema miradi hiyo inahitaji wataalamu wa TAKUKURU ambao watazuia rushwa.

"Msisubiri mhalifu atumie mbinu mbalimbali zikiwamo za mtandao hadi afanikiwe na kudhoofisha mradi husika. Mmepewa mafunzo hapa mzuie hilo lisifanyike ili thamani ya miradi iendane na fedha halisi," aliagiza.

Waziri Simbachawe alisema serikali imekuwa akitafuta fedha za maendeleo kutoka ndani na nje ya nchi, hivyo inastahili watendaji waadilifu, watakaosaidia adhma ya serikali kufanikiwa katika kuwaletea wananchi maendeleo. Kuhusu watumishi kuingia katika ajira kisha kutaka kuhama idara nyingine, alisema serikali imesimamisha utaratibu huo na badala yake, utafanyika katika utaratibu maalumu chini ya Katibu Mkuu Kiongozi.

"Ninyi mmeingia katika mfumo wa ajira, kulingana na taalumu zenu, wapo wanasheria, wahandisi, watu wa manunuzi, TEHAMA, hivyo mnapaswa kuisaidia serikali kwa uadilifu mkubwa. Hatutegemei mkaombe kuhama kwa maslahi yenu binafsi," alisema.

Kuhusu namna ya kutengeneza ushahidi kwenye kesi, Waziri Simbachawene aliwataka wataalamu hao kuwa makini katika kutengeneza nyaraka na vidhibitisho vitakavyoiwezesha Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashitaka (DPP) kuruhusu kufunguliwa kwa kesi husika.

Alisema kuna mifano michache ambapo kuwekuwapo na udhaifu katika kuandaa ushahidi, hatua inayosababisha Ofisi ya DPP kutoonyesha nia ya kuendelea na mashitaka licha ya kwamba, serikali imeshapata hasara katika miradi.

Akitoa taarifa ya mafunzo hayo, Mkurugenzi Mkuu wa TAKUKURU, Kamishna Salum Hamduni, aliwataka wahitimu hao kwenda kuleta tija katika maeneo watakayokwenda.

Mratibu wa mafunzo hayo, Richard Kiura, alisema wahitimu hao walipokelewa 396 na kati yao, 26 wanapaswa kurudia mitihani yao kwa mwezi mmoja.

Baadhi ya wazazi wa wahitimu hao, walisema mafunzo hayo yatasaidia kuleta tija katika kumaliza migogoro hasa ile ya maendeleo vijijini.


## NOTISI/TANGAZO

**LEGENDS AUCTION MART LTD, DESTENI COMPANY LIMITED, NUTMEG AUCTIONEERS & PROPERTY MANAGERS CO.LTD ,SALEI AUCTION MART LTD,HEDANE ENTERPRISES LTD, MASE INTERNATIONAL LTD,TAUSI AUCTION MART,MASETO AUCTIONEER AND DEBT COLLECTORS, JY AUCTIONEERS CO.LTD, NGOMENI AUCTION MART, REAL MASTER LTD,DRM AUCTIONEERS & CO.LTD, MAS AND ASSOCIATES CO.LTD,MELVA INTERNATIONAL LTD ,YONO AUCTION MART &CO.LTD ,SUMA JKT AUCTION MART COMPANY LTD,MAJEMBE AUCTION MART LTD, MABUNDA AUCTIONEER MART CO.LTD** kwa mamlaka tuliyopewa na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, chini ya AKIBA COMMERCIAL BANK PLC, tunatoa notisi ya kulipa deni kwa mdaiwa ndani ya siku 14 kuanzia tangazo hili, Vinginevyo, tutafanya Minada ya hadhara kama ratiba inavyoonyesha.

| TAWI ALILOKOPA | JINA LA MTEJA | AINA YA DHAMANA | JINA LA MWENYE DHAMANA | MAHALI DHAMANA ILIPO | TAREHE YA MNADA |
|---|---|---|---|---|---|
| MBAGALA | MAMU PHARMACY | NYUMBA ILIYOPO KWENYE KIWANJA NA.151,KITALU 'Q10' HATI NAMBA 143195-KIBAMBA | AHMAD KASSIM OMARY | KIBAMBA | 20/10/2023 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| KIJITONYAMA | NEZAK INVESTMENT LTD | 1.NYUMBA YENYE HATI NA. DSMT1019002 KIWANJA NAMBA P23439 KIFURU-KINYEREZI 2.NYUMBA YENYE HATI NA. 67242 KIWANJA NA. '637', KITALU 'F' BUHONGWA MWANZA 3..NYUMBA YENYE HATI NA. 70437 KIWANJA NA. '213', KITALU '14' BUNJU KINONDONI | 1. ZACHARIA ANTHONY KAPAMA 2. MARIANA ZACHARIAS BUKWIMBA 3.DAFROSA ATHONY KAPAMA | 1.KIFURU KINYEREZI-ILALA 2.BUHONGWA MWANZA 3.BUNJU KINONDONI | 20/10/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MAIN | TOMONI FARMS LIMITED | SHAMBA LENYE HATI YA MAUZIANO YA SERIKALI YA KIJIJI, EKARI 194 | FRANKLIN G. BAGALLA | KIJIJI CHA TOMONI-KIBITI RUFIJI | 17/10/2023 SAA 05:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| AGGREY | KOKUBELWA PAUL NGAMBEKI | KIWANJA | ANTHONY AARON ICHWEKELEZA | MPIJI MAGOE | 10/10/2023 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| UKONGA | JOFREY MTITU THEOFIRI | NYUMBA | JOFREY MTITU THEOFIRI | VIWEGE MAJOHE | 13/10/2023 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| KARIAKOO | OMARI SAIDI MAINGO | NYUMBA | OMARI SAIDI MAINGO | TAMBANI-MKURANGA | 17/10/2023 SAA 05:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| KARIAKOO | MEJO ENTERPRISES COMPANY LTD | NYUMBA | JOHN SEBASTIAN MBILINYI | MLONGANZILA | 23/10/2023 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| MBEYA | BAHATI YOHANA NYATO | NYUMBA YENYE LESENI YA MAKAZI | BAHATI YOHANA NYATO | LYAMKENA-MAKAMBAKO | 10/10/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MBEYA | FRENK SAMSON LEMAU | NYUMBA ZENYE HATI YA MAUZIANO | FRENK SAMSON LEMAU | SHEWA-MBEYA | 11/10/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MBEYA | KIVAULA MLIMKA LUHANGA | NYUMBA (2) ZENYE HATI MILIKI | KIVAULA MLIMKA LUHANGA | 1.MBEYA MJINI 2. TUNDUMA | 11/10/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MBEYA | VENANCE JISKAKA MWAKYABALA | NYUMBA YENYE HATI MILIKI | VENANCE JISKAKA MWAKYABALA | MWANJELWA , MBEYA MJINI | 11/10/2023 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MBEYA | EMANUEL MOYO MASETA | 1.NYUMBA (3) 2.KIWANJA | EMANUEL MOYO MASETA | 1.IFWEKENYE -MBOZI 2.SONGWE | 13/10/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MBEYA | NDIMBWELU BANDEKISYE KAFWENDA | NYUMBA | PAULO KALOTA NDAWILA | NZOVWE-MBEYA | 12/10/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MBEYA | IPYANA TIGER JUNIOR | NYUMBA | IPYANA TIGER JUNIOR | ILEMI-MBEYA | 16/10/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MBEYA | BRAITON REBEN MWANKEMWA | NYUMBA | BRAITON REBEN MWANKEMWA | IVUMWE | 16/10/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MBEYA | IDD SALUMU HUSSEIN | NYUMBA | EDITH JOSEPH CHIWAMILA | ISYESYE | 26/10/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| MBEYA | CHARLES JOHN ZIMBA | NYUMBA | CHARLES JOHN ZIMBA | ITEZI -MASHARIKI | 25/10/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| MBEYA | PRIVA EMANUEL SHIRIMA | NYUMBA YENYE HATI YA MAUZIANO | PRIVA EMANUEL SHIRIMA | KITETE-MBEYA | 20/10/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MBEYA | MARIAM BATON MWANDENENE | NYUMBA | VUMILIA ELIAS NYAGAWA | NGOSI- MWAKIBITI | 23/10/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| MWANZA | SONGALELI SAMA MZEE | KIWANJA | SONGALELI SAMA MZEE | BUSWELU MWANZA | 16/10/2023 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MWANZA | GRACE ADONIAS MTEGO | NYUMBA ILIYOPO KWENYE KIWANJA NA.22 KITALU 'N' HATI NA.4870 | BLASIUS SWAI KAGINA | BUNDA | 24/10/2023 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| MWANZA | ABAS HAMAD ISSA | NYUMBA YENYE HATI MILIKI | PETER NDULU MAHARAGE | MISUNGWI-MWANZA | 20/10/2023 SAA 12:00 MCHANA NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MWANZA | JUMANNE MOHAMED KAPOLI | NYUMBA YENYE HATI MILIKI | MATHIAS CHARLES NDETTO | KISESA-MWANZA | 15/10/2023 SAA 12:00 MCHANA NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MWANZA | MARIA JOHN PETRO | NYUMBA YENYE HATI MILIKI | JOHN PETRO KALISA | KILOLELI 'B' - MWANZA | 19/10/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MWANZA | MARTINA CORRONATUS RYOBA | 1.NYUMBA 2. KIWANJA | MARTINA CORRONATUS RYOBA | 1.IGELEGELE BUGARIKA 2. BUJINGWA-MWANZA | 19/10/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MWANZA | SELEMANI CHARLES MNIKO | NYUMBA | SELEMANI CHARLES MNIKO | MBUGANI -MWANZA | 17/10/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MWANZA | EMMANUEL LUKINDA LUTIMA | BUS TATA T847 DKN | EMMANUEL LUKINDA LUTIMA | MWANZA MJINI | 18/10/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MWANZA | JOSEPH MAKALA MAKALA | NYUMBA | JOSEPH MAKALA MAKALA | NYASAKA ILEMELA MWANZA | 13/10/2023 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MWANZA | JAMES JACOB KALULEMA | NYUMBA | JAMES JACOB KALULEMA | MAHINA KANYERERE-MWANZA | 13/10/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| ARUSHA | DISMAS JEROME MALLYA | NYUMBA | EMMANUEL NAFTALI NGUVILA | SOKONI I -ARUSHA | 23/10/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| ARUSHA | EMMANUEL LEJASA KIMATH | NYUMBA | EMMANUEL LEJASA KIMATH | SINONI -ARUSHA | 27/10/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| ARUSHA | LABANI SAMSONI MAKALA | NYUMBA | LABANI SAMSONI MAKALA | SINONI- ARUSHA | 16/10/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| ARUSHA | LESION JOSEPH MARTIN | NYUMBA | LESION JOSEPH MARTIN | SINONI- ARUSHA | 16/10/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| ARUSHA | MASANJA JAMES WANNA | KIWANJA | MASANJA JAMES WANNA | TERRAT - ARUSHA | 26/10/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| ARUSHA | LIGHTNESS JOSEPH MONGI | NYUMBA | LIGHTNESS JOSEPH MONGI | MURIET - ARUSHA | 23/10/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| ARUSHA | OLIVA STANLEY MNDEME | NYUMBA | STANLEY EMANUEL MNDEME | KIMANDOLU - ARUSHA | 26/10/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |

**MASHARTI YA MNADA**

1 Mnunuzi atalazimika kulipa 25% ya bei ya Nyumba, Kiwanja au Shamba ,papo hapo baada ya mnada kumalizika na 75% itakayobaki italazimika kulipwa ndani ya siku 14.

2 Ikiwa mnunuzi atashindwa kutimiza sharti lolote la mnada kuhusiana na malipo ya awali,hatarudishiwa pesa yoyote aliyokwisha ilipa.

3 Kwa mawasiliano zaidi; tupigie **simu no.0715868000/0714939933/0785242219/0754376493**

4 Iwapo ndani ya siku 60 mnunuzi hajakabidhiwa nyumba Benki itarudisha kiasi cha fedha kilichowekwa na mnunuzi Benki bila gharama yeyote.

217633802

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Makundi tumeyaona CAF, kazi kwenu Simba, Yanga

**JANA** ilichezeshwa droo ya makundi ya Ligi ya Mabingwa na Kombe la Shirikisho Afrika.

Mashabiki wa soka hapa nchini na Afrika Mashariki kwa ujumla walikuwa wakisubiri kwa hamu kujua timu zao zitapangwa kundi gani na wapinzani wapi.

Katika droo iliyochezeshwa jana jioni, wawakilishi wa Tanzania kwenye Ligi ya Mabingwa Afrika, Simba na Yanga zimejikuta zikiwa kwenye makundi mawili tofauti ya michuano hiyo.

Simba ambayo imeingia kwenye hatua hiyo kwa mara ya nne ndani ya miaka sita, imepangwa katika kundi B ikiwa na timu za Wydad Casablanca ya Morocco, ASEC Mimosas ya Ivory Coast pamoja na Jwaneng Galaxy ya Botswana.

Mabingwa watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Yanga wenyewe wamepangwa kwenye kundi D wakiwa na mabingwa watetezi wa michuano hiyo, Al Ahly ya Misri, CR Belouizdad ya Algeria na Medeama FC ya Ghana.

Kuwafahamu wapinzani wao mapema kwenye makundi yao kuna toa fursa sasa kwa klabu zetu hizi kujiandaa mapema kabla ya kuanza kwa michezo ya hatua hiyo.

Tunaamini kama Simba na Yanga zitaanza maandalizi yao mapema zina nafasi ya kuingia hatua inayofuata ya michuano hiyo mikubwa Afrika kwa ngazi ya vilabu.

Tunawakumbusha wawakilishi wetu, maandalizi yanatakiwa kufanyika mapema, maandalizi si tu mazoezini, lakini soka la sasa linatoa nafasi kwa benchi la ufundi kufuatilia wapinzani wao katika michezo wanayocheza.

Soka la sasa linahitaji ujuzi mkubwa wa kuwasoma wapinzani wako, mabenchi ya ufundi ya Simba na Yanga wana kazi hiyo ya kuwafuatilia na kuwasoma mapema wapinzani wao kabla ya kuanza kwa michezo ya hatua ya makundi.

Kama maandalizi yatafanywa katika kiwango cha juu, hakuna kitakachoshindikana kwa wawakilishi wetu hawa kufuzu hatua ya robo fainali ya michuano hii.

Simba wana uzoefu mkubwa wa hatua hii, imeshavuka mara mbili na kutinga hatua ya robo fainali, haitashangaza kuiona ikivuka tena na kutinga hatua hiyo.

Kwa Yanga licha ya kutokuwa na rekodi nzuri kwa miaka ya karibuni kwenye michuano hiyo, bado uzoefu wao wa kutinga hatua ya fainali ya Kombe la Shirikisho Afrika msimu uliopita inaweza ikawabeba na kufanya vizuri.

Tunasisitiza, hakuna kinachoshindikana, wawakilishi wetu wana nafasi ya kuvuka hatua hii, lakini hii itatokana na kujiandaa vizuri na kupambana uwanjani katika kila mchezo.

Katika hatua hiyo kila timu itacheza michezo sita, mitatu nyumbani na mitatu ugenini, kazi imebaki kwa wachezaji na mabenchi ya ufundi kuhakikisha wanafanya vizuri, watanzania na mashabiki katika ukanda huu wa Afrika Mashariki wanasubiri kuona nini timu zetu hizi zitafanya, tunazitakia kila la heri kwenye hatua hii ya makundi.


Hakuna ubishi tena kuwa kwa sasa soka la Tanzania katika ngazi ya vilabu inazidi kupaa Afrika.

Mwezi huu Simba itashiriki kwenye michuano mipya ya 'Africa Football League' ikiwa ndiyo timu pekee kwenye ukanda huu wa Afrika Mashariki na Kati kushiriki michuano hiyo.

Simba ina nafasi ya kuyatumia mashindano hayo yatakayoanza Oktoba 20 kujipanga kwa ajili ya hatua hiyo ya makundi ya Ligi ya mabingwa Afrika.

Lakini pia kwa Yanga, kwa kuwa wameshawajua wapinzani wao kwenye kundi lao, wanaweza kutumia mchezo wa ufunguzi wa Simba na Al Ahly kuwasoma wapinzani wao (Al Ahly) ambao wapo nao kwenye kundi moja la Ligi ya mabingwa Afrika.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko.** Dennis Ntaita. 0713 578284.
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Adam Fungamwango

### Pira 'gimbi' la Robertinho litaibeba Simba mikoani

**KUMEKUWA** na ukosoaji mkubwa juu ya soka linalochezwa na timu ya Simba kwa sasa chini ya kocha, Roberto Oliveira kutoka nchini Brazil.

Baadhi ya mashabiki wa timu hiyo bado wameonekana kutoridhishwa na aina yake ya uchezaji ambayo haina mbwembwe na nakshi nyingi kama ilivyokuwa kawaida ya timu hiyo kiasi cha kuzuka kwa jina la 'pira biriani.'

Hii ni aina ya soka ambalo wachezaji kabla ya kufika langoni kwa mpinzani wanakuwa wamepiga pasi nyingi kutoka maeneo mbalimbali ya uwanja.

Lakini pia mpira unakuwa umeshaguswa na wachezaji wengi.

Mwaka mmoja nyuma Simba walikuwa na aina hiyo ya mchezo ikiwa katika ubora na kiwango cha juu sana.

Hata kabla ya hapo, huu umekuwa ndiyo utamaduni wa klabu hiyo, wachezaji kuuchezea sana mpira kabla ya kufika kwa mpinzani.

Tangu ujio wa Robertinho kwa kiasi fulani amebadilisha mfumo wake. Haihitaji pasi nyingi kufika langoni mwa mpinzani.

Hili limekuwa likiwatesa baadhi ya mashabiki wa Simba ambao wamezoea lile soka lao la chenga nyingi na pasi fupi fupi.

Kiufundi ukiangalia falsafa ya Robertinho ni kwamba pamoja na baadhi ya mashabiki kutopendezewa lakini itawabeba sana kwenye viwanja vya mikoani ambavyo mara nyingi ubora wake umekuwa ni wa muda na havijakamilika kwa asilimia 100.

Ukitazama Simba imecheza mechi mbili ugenini kwenye viwanja vya aina hiyo visivyo na ubora mkubwa, ikishinda mechi zote mbili.

Simba iliifunga Mtibwa Sugar mabao 4-2 kwenye Uwanja wa Manungu, Complex, Turiani, na mechi ya juzi ilishinda mabao 3-1 dhidi ya Prisons.

Wachambuzi wanaomkosoa Robertinho wakae wakijua kuwa tangu atue nchini, si tu kwamba hajapoteza mechi yoyote, bali ana wastani mkubwa wa kushinda mechi za ugenini.

Wakati Simba inacheza soka lake 'biriani' na kushinda mechi zake zaidi Uwanja wa Benjamin Mkapa, haikuwa na matokeo mazuri ilipokuwa ikicheza mechi zake mikoani.

Na ukiangalia kiufundi utagundua wachezaji wake hawakuwa wakicheza kulingana na mahitaji ya uwanja. Waliendelea kupiga pasi fupi fupi na mbwembwe nyingi, wakati wapinzani wao walitumia mipira mirefu.

Hii ilikuwa ikiwachosha mno wachezaji na miaka ya nyuma Simba haikuwa na wastani mzuri wa kushinda ugenini kutoka na kutatizwa na uwanja, ambapo kwa kiasi kikubwa ilitokana na aina yake yenyewe ya uchezaji.

Hata wakati mwingine ubingwa ilikuwa inaukosa kutokana na kupoteza pointi, kufungwa ama sare kwenye viwanja vingi vya mikoani.

Wakati mashabiki wakimpigia kelele Robertinho lakini wanashindwa kujua kuwa ameonekana kuwa ndiyo mwarobaini wa timu hiyo kupata ushindi kwenye viwanja vya mikoani na kwa mahesabu ya ligi ndivyo vinavyotoa bingwa.

Simba imekuwa mhanga hata kwenye Uwanja wa Sokoine jijini Mbeya dhidi ya Prisons na Mbeya City kwa misimu kadhaa, ilikuwa inapoteza mechi zake, au kudondosha pointi mbili kwa sababu ya aina ya uchezaji wao.

Kwa sasa Simba wakifika kwenye viwanja vya aina hiyo hawana mbwembwe nyingi, pasi mbili tatu unapigwa mpira mrefu kwenda kwa mabeki wao Mohamed Hussein 'Tshabalala' na Shomari Kapombe ambao wanapanda kwenda kusaidia mashambulizi na kupiga krosi, kina Clatous Chama na Saido Ntibazonkiza wakiingia kati kumsaidia mshambuliaji.

Mfano mzuri umeonekana katika mechi dhidi ya Prisons ambayo ilikuwa ikiisumbua sana Simba katika uwanja huo.

Na hata Kocha Fred Felix Minziro alitarajia wapinzani wake watacheza kama wanavyofanya miaka yote, pasi fupi fupi.

Kuna wakati hasa kipindi cha pili, timu zote zilifanana kwa kupiga pasi ndefu nyuma ya safu ya ulinzi, kitu ambacho kiliwasumbua sana Prisons kwa sababu hawakutarajia hilo.

Kama Simba itaendelea kucheza hivi kwenye viwanja vya ugenini, itavuna pointi nyingi na inaweza kujiweka kwenye nafasi nzuri ya kutwaa ubingwa kama itakuwa ikishinda pia kwenye uwanja wake wa nyumbani, Benjamin Mkapa ambao utafunguliwa baada ya Oktoba 20.

# Maktaba zapunguza utoro wa wanafunzi

**Na Julieth Mkireri,**
MKURANGA

UWAPO wa maktaba shuleni ikiwa na vitabu vingi vya hadithi inaelezwa kuwa kichocheo cha wanafunzi kupenda kusoma na kujifunza na kuachana na tabia ya utoro.

Mwanahamis Selemani, mkazi wa Mkuranga, alibainisha hayo jana wakati wa Tamasha la Usomaji lililoandaliwa na Shirika la Kimataifa la Room to Read lililofanyika katika Shule ya Msingi Mkuranga.

Alisema kitendo cha kuwa na maktaba kimekuwa kichocheo cha wanafunzi kupenda kujua kusoma kwa haraka na wengine kuachana na uvivu wa kwenda shule, jambo ambalo limeleta mabadiliko ya kuwa na wasomi wengi baadaye.

"Wakati mwingine mtoto anaumwa na hali haijaimarika lakini analazimisha kwenda shuleni ili wenzie wasimpite kwenye masomo. Ninawashukuru Room to Read kwa kutambua umuhimu wa maktaba shuleni," alisema.

Meneja Uendeshaji wa mradi huo, Agripina Kadama, alisema katika kutekeleza mradi wa usomaji, shule za msingi 35 za Halmashauri ya Mkuranga zimefikiwa.

Pia alisema wametoa usaidizi wa kitaalamu kwa walimu kuhusiana na uwezeshaji wa elimu ya stadi za maisha na elimu ya fedha katika shule za msingi 19 na mafunzo ya KK kwa darasa la kwanza ambapo walimu 113 walinufaika.

"Pia mafunzo ya uendeshaji wa vipindi vya maktaba, mbinu za ujifunzaji na ufundishaji, mbinu za sauti yote yalitolewa kwa walimu wa darasa la kwanza kwa shule za mradi, walimu wa somo la kiswahili, maofisa elimu kata na wadhibiti ubora walinufaika," alisema.

Kadama alisema vitabu 7,906 vya KK kwa wanafunzi wa darasa la kwanza pamoja na vya hadithi za watoto 53,319 na miongozo 242 ya KK na uendeshaji maktaba vilitolewa.

Kadhalika alisema kupitia mradi wa elimu kwa msichana, msaada wa kitaaluma wa elimu ya stadi za maisha na fedha kwa walimu 29 walinufaika.

Akizungumza kwa niaba ya Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Mkuranga, Ofisa Elimu Watu Wazima, Regina Masyole, alisema mwanafunzi anapokuwa darasa la kwanza na la pili hujifunza stadi za kusoma na kuandika darasani.

Hata hivyo, alisema kujua kusoma na kuandika pekee hakutoshi kumfanya wanafunzi kuwa msomaji mahiri na mwenye kupenda kujisomea, hivyo mwanafunzi huhitaji kupata fursa ya kujisomea vitabu kwenye maktaba ili kukuza stadi ya usomaji na kujenga tabia ya usomaji.

# Waziri Silaa ataka mfanyabiashara asibughudhiwe

**Na Munir Shemweta,**
MOSHI

WAZIRI wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Jerry Silaa, ameagiza mmiliki wa mgahawa wa Fresh katika Manispaa ya Moshi, asisumbuliwe na badala yake asaidiwe ili kulitumia eneo lake kulingana na matumizi anayohitaji.

Silaa alitoa agizo hilo juzi wakati akikagua maeneo mbalimbali ya Halmashauri ya Manispaa ya Moshi yanayolalamikiwa kujengwa au kutumiwa kinyume cha taratibu ikiwa ni juhudi zake za kuhakikisha uendelezaji miji unafuata sheria na kanuni.

Akiwa katika katika eneo hilo, Waziri Silaa alielezwa na Ofisa Mipango Miji wa Manispaa ya Moshi, Richard Emily, kuwa mwaka 1959 kiwanja kinachomilikiwa na mfanyabiashara huyo, awali kilimilikishwa kwa Moshi Trading Company Limited na baadaye kubadilishwa umiliki na sasa kinamilikiwa na Baraka Mallya.

Kwa mujibu wa ofisa huyo, mwaka 1987 yalifanyika marekebisho ya upimaji wa kiwanja hicho ya kumegwa sehemu ya kiwanja yenye ukubwa wa mita za mraba 483 kama eneo la wazi.

"Eneo hili kwa mujibu wa mchoro ya mipango miji ulioidhinishwa na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makaz mwaka 1997, umetenga viwanja viwili vya matumizi ya makazi pekee," alisema Emilly.

Hata hivyo, alisema mwaka 2001 Halmashauri ya Manispaa ya Moshi kwa kushirikiana na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, iliandaa mpango wa uendelezaji eneo la mjini kati na sehemu ya kiwanja hicho lilipendekezwa kuwa eneo la wazi.

Kutokana na maelezo hayo, Waziri Silaa alishangazwa na namna halmashauri inavyoshughulika na suala la umiliki wa kiwanja cha mfanyabiashara huyo.

"Ile hati haikuwahi kuwa 'surrended' (kusalimishwa). Hamkutoa hati mpya, mtu anamiliki eneo lake na analipia kodi ya pango la ardhi lote. Sasa eneo la wazi mnalitoa wapi?" alihoji Waziri Silaa.

Aliitaka Halmashauri ya Manispaa ya Moshi kupitia watendaji wa sekta ya ardhi kuacha kumsumbua mfanyabiashara huyo kwa kuwa ana haki na anamiliki eneo hilo kihalali.

Waziri alisema amesema kama kuna uhitaji wa mabadiliko ya matumizi ya kiwanja basi wamsaidie na waondoe taharuki kwa wananchi. Waziri Silaa aliwahakikishia wananchi kuwa akiwa Waziri wa Ardhi, ataendelea kutenda haki bila kujali cheo, rangi wala sura kwa kuwa ameteuliwa na Rais Samia Suluhu Hassan kuhudumia wananchi wote.

Alimtaka mmiliki wa kiwanja hicho kwenda kwa Kamishna wa Ardhi Msaidizi Mkoa wa Kilimanjaro, Rehema Jato, ili asaidiwe kama ni kubadilisha matumizi ya biashara na iwapo watu wa mji wa Moshi wataona inafaa basi asaidiwe katika hilo.

Katika ziara yake ya siku moja mkoani Kilimanjaro, Waziri Silaa mbali na kutembelea eneo la mgahawa, alikagua pia eneo la Mawenzi Marathon Shabaha, kata ya Mawenzi panapojengwa kituo kidogo cha mafuta pamoja na uwanja wa ndege Korongoni zinapojengwa nyumba tatu za makazi zisizokuwa na hati.

Waziri alihitimisha ziara yake kwa kuzungumza na watumishi wa sekta ya ardhi na kuwataka kufanya kazi kwa weledi na kutoa huduma nzuri kwa wateja.



Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Jerry Silaa (kulia), akiangalia ramani wakati akikagua ujenzi usioendana na mipango miji, Manispaa ya Moshi mkoani Kilimanjaro juzi. **PICHA: WANMM**

# TFS yavutia uwekezaji utalii katika vivutio, hifadhi za asili

**Na Elizabeth Zaya**

WAKALA wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS) imehamasisha uwekezaji katika eneo la utalii wa vivutio na hifadhi asilia.

Naibu Kamishna wa Uhifadhi wa TFS, Zainabu Bungwa, alitoa hamasa hiyo jana wakati wa upandaji wa mikoko na miti katika fukwe ya Kunduchi Beach, kazi iliyofanywa na wajumbe wa kongamano la tatu la kimataifa la viongozi vijana na mabadiliko ya tabianchi.

Kongamano hilo linatarajiwa kumalizika leo jijini Dar es Salaam, likijumuisha vijana zaidi ya 300 kutoka nchi 24 duniani.

Bungwa alisema katika kupambana na uharibifu wa mazingira na kuendelea kulinda maliasili na hifadhi asilia, kuna haja ya kuongeza nguvu katika uwekezaji zaidi katika eneo hilo.

"Tunawakaribisha wawekezaji kuja kuwekeza katika eneo hili na tunaamini kwa kufanya hivi, itasaidia hata kupambana na mabadiliko ya tabianchi ambayo kwa kiwango kikubwa, chanzo chake ni uharibifu huo wa mazingira," alisema Bungwa.

Pia alisema kuna haja ya kuweka nguvu kwa vijana kwa kuwaelimisha kuhusu umuhimu wa uhifadhi wa mazingira na faida zake.

"Tunataka vijana walirithishwe zaidi utunzaji wa mazingira kwa kuwa, hawa ndiyo viongozi wajao tunaowategemea ambao tunaamini kwamba, wanapoiva vizuri katika eneo hili, dunia itakuwa salama zaidi kwa kuishi kwa kuwa, watazidi kurithisha kwa wengine," alisema nak uongeza kuwa TFS itaendelea kupandisha hadhi hifadhi mbalimbali za misitu nchini.

Mwanzilishi na Mkurugenzi Mtendaji wa Kituo cha Uongozi wa Vijana wa Kimataifa, Ejaj Ahmad, alisema mabadiliko ya tabianchi yanatesa dunia, hivyo kila nchi inapaswa kuongeza juhudi za kupambana na uharibifu wa mazingira na kuweka mikakati imara ya kuyatunza.

"Ndiyo maana katika juhudi za mapambano hayo, tumewakutanisha vijana hawa kutoka nchi mbalimbali kuja kuwapa mbinu za kupambana katika eneo hilo, tukiamini hili ni kundi kubwa na lenye nguvu," alisema Ahmad.

Mwanaharakati wa mazingira kutoka Zambia, Martin Mulenga, alisema wanaamini yale ambayo wamejifunza katika kongamano hilo, yatakuwa chachu ya kuendelea kutoa elimu kwa jamii kuhusu umuhimu wa utunzaji wa mazingira.

"Tumejifunza mengi sana, namna Tanzania inafanya katika kupambana na uharibifu wa mazingira hususani kwenye mikakati yake ya kupanda miti, utunzaji na uendelezaji wa misitu asilia, na kama mabalozi wa mazingira, tumelibeba hili na tutakwenda kufanyia kazi huko tuendako," alisema Mlenga.

# PPRA yaokoa bil. 2.6/- ununuzi wa umma

**Na Joseph Mwendapole**

MAMLAKA ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma (PPRA) imeokoa zaidi ya Sh. bilioni 2.6 kwa kuzuia malipo yaliyokiuka utekelezaji wa mkataba katika ununuzi wa umma.

Pia mamlaka hiyo imeokoa fedha hizo kwa kubaini njama zilizopangwa na baadhi ya wazabuni kukwepa kulipa kodi ya ongezeko la thamani (VAT).

Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi PPRA, Dk. Leonada Mwagike, alisema hayo alipokuwa akikabidhi ripoti ya ukaguzi katika ununuzi serikalini kwa mwaka wa fedha wa 2022/23.

Alikuwa akikabidhi ripoti hiyo juzi kwa Naibu Waziri wa Fedha, Hamad Hassan Chande, kwenye hafla iliyofanyika jijini Dodoma.

Dk. Mwagike alisema PPRA ilibaini hayo wakati wa utekelezaji wa majukumu yake katika ukaguzi wa taasisi za serikali, mashirika ya umma na Wizara ambapo jumla ya taasisi 180 zilikaguliwa na ukaguzi huo ulijikita kuangalia taratibu za ununuzi na utekelezaji wa mikataba.

Alisema kutokana na ukaguzi uliofanyika, PPRA ilibaini baadhi ya makandarasi walikwepa kulipa VAT katika kazi walizozifanya serikalini.

Kwa mujibu wa Dk. Mwagike, hali hiyo ilisababisha PPRA kuelekeza wasilisho la stakabadhi hizo kabla ya mchakato wa ukaguzi kuisha ambapo jumla ya stakabadhi zenye thamani ya shilingi milioni 290 ziliwasilishwa. "Fedha zote hizi zilizopatikana kutokana na malipo ya kodi ya ongezeko la thamani zimerudishwa serikalini," alisema.

Alisema fedha nyingine zilizookolewa zilitokana na malipo yaliyofanyika kwa mtoa huduma ambayo hayakuwa sahihi na kwamba malipo hayo yenye thamani ya shilingi milioni 233 yalirejeshwa serikalini.

Pia alisema malipo yenye thamani ya Sh. bilioni 1.7 yaliokolewa kutokana na kusitisha malipo ya huduma iliyotolewa chini ya kiwango kwa moja ya taasisi za umma hali iliyosababisha PPRA kuelekeza taasisi husika kukatisha mkataba na mzabuni. Dk. Mwagike alisema licha ya fedha hizo kurudishwa serikalini kwa ajili ya matumizi mengine ya maendeleo, PPRA pia imemfungia mzabuni mmoja ambaye alihusika moja kwa moja na makosa ya kutoa huduma chini ya kiwango na kutaka kuisababishia Serikali hasara.

Alisema mzabuni huyo hataruhusiwa kutoa huduma yoyote serikalini na kwamba katika ripoti hiyo, PPRA ilipendekeza hatua mbalimbali kuchukuliwa kwa taasisi ambazo zimeisababishia serikali hasara.

"Mamlaka inatoa mapendekezo mbalimbali kwa taasisi nunuzi husika ikiwa ni pamoja na kuchukua hatua za kinidhamu kwa watumishi waliohusika na mchakato wa ununuzi iliyosababisha hasara kwa Serikali," alisema Dk. Mwagike.

Hiyo ni ripoti ya 17 kuwasilishwa kutokana na tathmini ya mwaka ya utendaji kwa taasisi za umma ikiweka tamati ya ripoti zilizowasilishwa mbele ya Waziri wa Fedha na kuanzia mwaka wa fedha 2023/2024 ripoti hiyo rasmi itakuwa ikiwasilishwa moja kwa moja kwa Rais.



Mkurugenzi Mkuu wa kampuni ya TotalEnergies Marketing Tanzania Ltd, Mamadou Ngom (katikati), akikabidhi koti la kuakisi mwanga 'reflector' kwa Mrakibu Msaidizi wa Polisi, Asulwisye Mwakyonike wakati wa uzinduzi wa programu ya usalama barabarani inayoitwa VIA, katika Shule ya Msingi Buza, jijini Dar es Salaam juzi. Kushoto ni Mkuu wa Sheria, Mashirika, Rasilimali Watu na Utawala wa kampuni hiyo, Getrude Mpangile. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Tanzania yashiriki mkutano kuboresha makazi

**Na Mwandishi Wetu,** ALGERS

UJUMBE wa Tanzania unaohudhuria Mkutano Mkuu wa dharura wa Shirika la Makazi Afrika (Shelter Afrique) unaofanyika jijini Algiers umekutana na maofisa wa Ubalozi wa Tanzania nchini Algeria ili kupata uzoefu wa uendelezaji wa Miji na Makazi unaofanyika katika taifa hilo.

Akizungumza katika kikao hicho kilichofanyika ubalozini eneo la Hydra jijini humo, kiongozi wa msafara huo,

Deogratius Kalimenzi, ambaye pia ni Mkurugenzi wa Maendeleo ya Miji na Vijiji wa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, alisema Tanzania ni mwanachama wa Shirika hilo na lengo la kikao hicho cha dharura ni kufanya mabadiliko makubwa ya kiutendaji ya kitaasisi ili hatimaye liingie kwenye mfumo wa kuwa benki ili kubeba jukumu kubwa la kuhudumia nyumba na maendeleo ya makazi katika Afrika.

Alisema kikao hicho kinaenda kupanua maeneo ya kuboresha makazi ya watu na shirika linabidi liwe na fedha za kugharamia miradi ya maendeleo.

Kadhalika hoja mbalimbali zitajadiliwa ikiwamo namna ya hisa za shirika hilo zitakavyokuwa kwa kila nchi wanachama na kushirikisha wadau wengine zikiwamo taasisi zingine.

Aidha, ajenda zingine ni namna mamlaka ya kuajiri na kuanzishwa kwa Bodi ya Ushauri ya Shirika hilo itakayosimamiwa na mawaziri sita wa nchi wanachama wanaosimamia masuala ya fedha na uchumi.

"Tanzania ina changamoto ya makazi na kwa mujibu wa Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2022 iliyojumuisha sensa ya majengo Tanzania ina majengo milioni 14 na asilimia 91 ni kwa ajili ya makazi."

Kwa mujibu wa sensa hiyo ina watu milioni 61.7 idadi hiyo inaongezeka kwa asilimia 3.2 na kuwa kuna upungufu wa nyumba milioni 3.8 na kila mwaka mahitaji yanaongezeka kwa idadi ya nyumba 390,000 na uwezo wa taasisi ndani ya nchi wa kujenga nyumba ni asilimia 0.02 ya mahitaji ya nyumba kwa mwaka.

Alisisitiza kuwa Tanzania inahitaji kuwa na teknolojia ya ujenzi wa nyumba inayokubalika na jamii na kuwa na vyanzo vya uhakika vya fedha za kugharamia ujenzi.

Vile vile, amefurahishwa na ujenzi wa majengo ya ghorofa yaliyojengwa katika Jiji la Algiers na kwamba Tanzania imeanza kuweka msisitizo wa ujenzi wa majengo ya ghorofa ili kupunguza gharama za uwekaji wa miundombinu na kusambaza huduma muhimu za kijamii.

"Tanzania inahitaji shirika hilo la nyumba Afrika ili kufungua milango ya uwekezaji katika sekta ya nyumba na makazi," alisisitiza.

Alisema nchi imeshanufaika na mikopo kutoka Shelter Afrique na Shirika la Nyumba la Taifa lilipata mkopo wa kujenga nyumba za gharama nafuu wa Sh. trilioni 15.

Aliuomba Ubalozi wa Tanzania Algeria kuwezesha ujumbe wa Tanzania kukutana na Wizara ya Nyumba na Maendeleo ya Miji ya Algeria ili kufahamu namna walivyofanikiwa kujenga nyumba 40,000 kwa mwaka na kuwa na miundombinu madhubuti katika miji mingi ya nchi hiyo.

Akijibu maombi ya ujumbe huo, Ofisa Balozi wa Tanzania Algeria aliyemwakilisha Balozi, Must Suleyman, alisema kuwa Algeria imepiga hatua kutokana na serikali yao kuwekeza katika ujenzi wa miji na miundombinu.

Alisema ubalozi huo umefanya mashauriano na nchi ya Algeria na kuweka makubaliano kupitia tume ya pamoja iliyoundwa kusaidia kubadilishana mambo mbalimbali ikiwamo sekta ya nyumba, makazi na mafuta.

Wamekubali kuendelea kuishawishi nchi hiyo kusaidia Tanzania teknolojia na fedha za kufanya maendeleo ya nyumba nchini Tanzania.

Mkutano huo wa Shelter Afrique umefunguliwa jana jijini Algeria na unahusisha nchi wanachama 45 wa nchi za Afrika ikiwamo Tanzania.

Oktoba 5, mkutano huo unatarajia kupitisha maazimio kadhaa yatakayowezesha kulibadili shirika hilo na kuwa Benki ya Maendeleo ya Shelter Afrika.

# Mnigeria amrithi Mtanzania, AFF

**Na Emmaloveness Gaston**

JUKWAA la Misitu Afrika (AFF), limemteua Prof. Labode Popoola wa Nigeria kuwa Mtendaji Mkuu baada ya Mtanzania Prof. Godwin Kowero, kumaliza muda wake.

Kwa mujibu wa taarifa kwa umma, Bodi ya AFF iliyokutana hivi karibuni, ilimteua Prof. Labode ambaye ni mtaalamu wa misitu iliyefanya kazi katika maeneo mbalimbali ndani na nje ya bara la Afrika.

Bodi hiyo ilisema lengo ni kuhakikisha taasisi hiyo inafanyakazi kwa ufanisi na kuendelea kutambua mchango wa misitu na miti Afrika.

Taarifa hiyo ilibainisha kuwa Prof. Labode atakuwa na jukumu la kudumisha umuhimu na kutambua mchango wa misitu na mazingira barani Afrika kwa manufaa ya jamii yote na taifa kwa ujumla.

"Tangu Oktoba mosi, mwaka huu, Labode ndiye Mtendaji Mkuu-Mkurugenzi, anayechukua nafasi iliyoachwa na Prof. Kowero ambaye ameiongoza na kuisimamia AFF tangu kuanzishwa kwake mwaka 2007," ilifafanua taarifa.

"Atakuwa na jukumu la kuhakikisha ofisi ya AFF inafanya kazi kwa ufanisi katika kusaidia harakati za pamoja ikilenga zaidi kutambua umuhimu na mchango wa misitu na miti kwa watu wa Afrika na mazingira yao," ilibainisha taarifa hiyo.

Prof. Labode ana shahada ya Uzamili katika Uchumi wa Misitu ya Chuo Kikuu cha Ibadan na aliwahi kuwa Mkurugenzi wa Mtandao wa Suluhu za Maendeleo Endelevu wa Umoja wa Mataifa Nigeria 2019.

Aidha, taarifa hiyo ilifafanua kuwa AFF katika kutambua mchango wa misitu na miti barani Afrika na uhitaji wa utafiti imeongeza idadi ya wafanyakazi kutoka mmoja kipindi inaanzishwa na kufikia 10 hadi sasa.

"Taasisi imekua kutoka mfanyakazi mmoja hadi watafiti watatu mwaka 2019. Sasa ina wafanyakazi wa kudumu 10 ambao sita kati yao wakiongoza kazi za sayansi za taasisi na kuungwa mkono na wataalamu wanne wa kiufundi," ilielezea taarifa hiyo.

Vilevile taasisi hiyo kwa niaba ya wanachama na Baraza la Uongozi imemshukuru Prof. Kowero kwa kujitoa, utaalamu na mchango wake katika kipindi chote cha uongozi wake ndani ya AFF.



# Wakutana kutatua matatizo ya kiafya

**Na Mwandishi Wetu**

ZAIDI ya wataalamu 100 wamekutana kujadili namna ya kutatua matatizo yanayoikabili huduma ya utangamano kwa watu wenye mahitaji maalum kiafya nchini.

Wataalamu hao ni wanaotoa huduma ya tiba ya kuzungumza na sikizi, tiba ya viungo, tiba ya kazini, afya ya akili na madaktari wa mifupa.

Akizungumza wakati wa mkutano huo, mwazilishi wa Taasisi ya Rehab Health, Remla Shirima, alisema kwa sasa nchini kuna uhaba wa wataalamu wa huduma za utangamano ambao hawazidi 2,000.

"Serikali imejikita zaidi katika uwezeshaji na uwekezaji katika huduma za utengamano. Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu, wakati anawasilisha bajeti yake ya wizara bungeni Mei mwaka huu alitaja vipaumbele 14 vya Wizara ya Afya ni pamoja na upatikanaji na utoaji wa huduma za utengamao," alisema Remla.

Alisema kutokana na hali hiyo, Rehab Health imeona ni vyema kuungana na serikali katika kuunga mkono na kutoa huduma hiyo ifike hadi vijijini katika vituo vya afya.

Shirima alisema lengo lingine ni kuhakikisha mafunzo yanapatikana kwa wataalamu kwa sababu idadi ya madaktari katika sekta hiyo ni wachache.

Alisema pia wanahakikisha kunakuwapo na maeneo maalumu ya kupata huduma hiyo katika hospitali pamoja na vifaa vya matibabu.

Lengo la Rehab Health, alisema ni kuhakikisha kunakuwapo na upatikanaji wa vifaa saidizi, upatikanaji wa mafunzo kwa wataalamu wa kutoa tiba hiyo pamoja na kushirikiana na wadau wengine wa sekta ya afya ili kukuza sekta hiyo.

Mratibu wa Huduma za Afya Wazee (Idara ya Tiba) Wizara ya Afya, Dk. Msafiri Kabulwa, alisema serikali imeweka mkakati wa kuhakikisha huduma za utangamano zinapatikana maeneo yote.

Dk. Kabulwa alisema bado kuna changamoto ya kufikisha huduma za utangamano kwa watu wenye mahitaji maalum kiafya katika ngazi ya vituo vya afya, lakini kwa sasa huduma hiyo inapatikana pekee katika Hospitali ya Taifa, mikoa na wilaya.

# Wazee walia mzigo kutunza wajukuu

**Na Thobias Mwanakatwe,**
MANYONI

WAZEE wa Mkoa wa Singida wamekemea tabia ya watoto wao kuwatelekezea wajukuu na wao kubaki mijini kula maisha bila kutoa fedha za matunzo hali inayoongeza ugumu wa maisha kwao.

Wazee hao waliyasema hayo juzi kwenye maadhimisho ya Siku ya Wazee Duniani yaliyofanyika kimkoa wilayani hapa.

Mwenyekiti wa Baraza la Wazee Wilaya ya Iramba, Israel Msengi, alisema hivi sasa kumezuka tabia watoto wakienda mijini wanazaa watoto na baadaye wanapeleka kwa bibi na babu wawalee huku wenyewe wakibaki mijini kuendelea na starehe.

"Si kwamba wajukuu zetu ni wabaya hapana.

Ni wazuri lakini tatizo wazee wanapelekewa wajukuu hata uwezo hawana wa kuwatunza. Niwaombe watoto wetu kwa kuwa tumeshazeeka wakipata watoto wawalee wenyewe na si kuja kuwatelekeza kwa bibi na babu," alisema.

Katika maadhimisho hayo, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Manyoni, Jimson Mhagama, ambaye alimwakilisha Mkuu wa Mkoa wa Singida, Peter Serukamba, aliwakabidhi wazee 100 kadi za Bima ya Afya ya Jamii iliyoboreshwa (iCHF).

Akizungumza na wazee hao, Mhagama alisema suala la wazee kupatiwa vitambulisho vya matibabu ni agizo la serikali ili kuhakikisha wanatambuliwa na kupewa huduma stahiki.

Alipongeza hatua nzuri iliyofikiwa katika uundwaji wa mabaraza ya wazee 637 kati ya hayo mabaraza 151 sawa na asilimia 24 yamejengewa uwezo katika mkoa wa Singida ili kuhakikisha huduma na maslahi ya wazee yanapatikana.

Pia aliwaagiza wakurugenzi wote wa halmashauri kuhakikisha mabaraza ya wazee yanafanya vikao vyao kila robo mwaka kama miongozo inavyoelekeza ili kuwezesha ufanisi katika kazi zao.

Alitoa rai kwa jamii hasa ndugu wa karibu kuacha tabia ya kuwanyang'anya Wazee maeneo yao ya ardhi na nyumba jambo linalosababisha wazee kukosa mwelekeo kwani kufanya hivyo ni kinyume cha sheria na wale watakaobainika sheria itachukua mkondo wake.

Kuhusu malezi ya watoto, Mhagama alisisitiza umuhimu wa wazazi kuwalea watoto wao ili kuwajengea stadi mbalimbali za maisha na kufanya wawe raia bora.

Mhagama alitoa wito kwa vijana kuwatunza wazee wao ambao ni hazina kwa kuwatimizia mahitaji yao mbalimbali ikiwemo chakula ili kuepuka Wazee kuzunguka mitaani wakiombaomba.

Aliwakumbusha na kuwaomba wazee kuendelea kusisitiza suala la malezi chanya kwa watoto na maadili mema kwa vijana ili kujenga jamii isiyokuwa na mmomonyoka wa maadili.



Mkunga Kiongozi wa wodi ya mama na mtoto hospitali ya CCBRT, Intisar Ahmed akimwelekeza kwa vitendo, Emanuel Goodluck kuhusu umuhimu wa mtoto kukaa ngozi kwa ngozi na mama yake saa moja baada ya kuzaliwa na uwepo wa mwenza au msaidizi wakati wa kujifungua, alipotembelea banda la hospitali hiyo, katika Jukwaa la Mwaka la Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, jijini Dodoma juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Asasi kujenga shule lugha za alama

**Na Renatha Msungu,**
DODOMA

SHIRIKA lisilo la kiserikali la Tanzania Chesire Foundation (TCF) linatarajia kujenga shule ya lugha za alama mkoani Dodoma itakayotoa

mafunzo kwa kada mbalimbali ili kurahisisha mawasiliano kwa viziwi.

Akizungumza na waandishi wa habari jana katika maonyesho ya Wiki ya Asasi za Kiraia, jijini hapa, Mwenyekiti wa Bodi ya TCF, Steven Masangia, alisema shule hiyo inatarajia kujengwa katika eneo la Nala ili kusaidia kuondoa tatizo la mawasiliano kwa viziwi kwenye maeneo ya kutoa huduma za kijamii.

Akitolea mfano katika nyumba za ibada, alisema endapo viongozi wa dini wakijua kufundisha au kuhubiri kwa lugha za alama, itakuwa imesaidia jamii hiyo nao kushiriki ibada kama ilivyo jamii nyingine.

"Tunaishukuru sana serikali kwa kutupatia eneo hilo,tunaomba wadau wengine wajitokeze kutusaidia fedha kwa ajili ya kujenga shule hiyo ambayo ni ya muhimu katika taifa letu," alisema Masangia.

Alisema katika ujenzi huo, kutakuwa vitu mbalimbali ambavyo vitawekwa ili kuhakikisha wanakidhi vigezo vinavyohitajika katika ujenzi wa

shule hiyo ambayo itasaidia kutoa mafunzo kwa watu mbalimbali.

Kadhalika, alisema TCF inatarajia kutoa mafunzo ya lugha za alama kwa wanahabari na wachungaji na watumishi wa dini zote ili kutoa urahisi wa

kuwasiliana na jamii ya watu wenye ulemavu wanapotoa ibada za kanisani na misikitini.

Mratibu wa Miradi wa TCF, Wenance Mhombwe, alisema shirika hilo pamoja na kuwawezesha kiuchumi watu wenye

ulemavu, limekuwa pia likiviunganisha vikundi hivyo na serikali kwa ajili ya kupata mikopo mbalimbali ambayo inalenga jamii hiyo na hadi sasa zaidi ya vikundi 30 vimeundwa.

Alihimiza wazazi na walezi kutowafungia watu wenye ulemavu badala yake wawatoe kwa ajili ya kwenda kuwezeshwa kiuchumi na mashirika mbalimbali yasiyo ya kiserikali na serikali kwa ujumla.





# RC apiga 'stop' uvaaji vimini, nguo mbano

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MKUU wa Mkoa wa Kaskazini Unguja, Ayoub Muhammed Mahmoud, amepiga marufuku uvaaji wa mavazi ambayo ni kinyume cha maadili katika mkoa huo, vikiwamo vimini na nguo zinazobana.

Aliyasema hayo juzi wakati akizungumza na wananchi wa vijiji vya Kendwa, Kilindi na Tazari wakati wa mwendelezo wa mikutano yake ya kusikiliza kero za wananchi katika mkoa huo.

Ayoub alitoa agizo hilo baada ya kupokea malalamiko ya wananchi wa vijiji hivyo kuhusu kuporomoka kwa maadili ikiwamo uvaaji wa nguo zinazokwenda kinyume cha maadili pamoja na uwapo wa biashara za ukahaba.

Ayoub alitoa wiki moja kwa wamiliki wa hoteli za kitalii katika mkoa huo kuweka mabango maalum ambayo yatakuwa na ujumbe ya kwamba ni marufuku kutembea katika makazi ya wananchi wakiwa wamevaa mavazi yasiyo na staha.

"Niwatake wenye hoteli kuwaelekeza wageni wao kwamba miongoni mwa utamaduni wa Zanzibar wanapotoka nje ya hoteli kuvaa mavazi ya heshima na ni marufuku kuvaa nguo za kubana na vimini,' alisema.

Ayoub aliwaagiza askari wa ulinzi shirikishi kuwachapa viboko wale wote watakaokiuka agizo hilo la kutovaa nguo za heshima.

Alisema wanatamani kuwa na wageni na watalii kutoka mataifa mbalimbali duniani lakini wanapaswa kuheshimu mila na desturi na wakishindwa kufanya hivyo ni vyema kuwaondoa.

"Tumeitisha utalii kwa lengo la kuimarisha uchumi wa nchi yetu wala si kwa lengo la kuvuruga mila, silka na utamaduni wetu," alisema Ayoub.

Awali, wananchi wa vijiji hivyo walisema changamoto kubwa ni kuporomoka kwa maadili kulikochangiwa na sekta ya utalii. Vijiji hivyo vimezungukwa na hoteli nyingi za kitalii.

Walisema si wageni wote wanaofika katika hoteli hizo wenye lengo zuri bali wengine huchangia katika kuharibu mila, silka na utamaduni kwa sababu baadhi yao hujihusisha na biashara za ukahaba.

"Utamkuta mgeni anatembea mitaani akiwa amevaa nguo za ndani tu, hajui kwamba tuna tamaduni zetu hapa. Unadhani mtoto akiona hali kama hiyo tunamfundisha nini? Lazima tuhakikishe huu utalii hauathiri utamaduni wetu," alisema Makame Mcha, mkazi wa kijiji hicho.

Kaskazini Unguja ni mkoa unaoongoza Zanzibar kwa kuwa na hoteli nyingi za kitalii na ni mkoa ambao una vivutio vingi vya utalii ikiwemo fukwe.



Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Albert Chalamila (kulia), akipokea vifaa vya hospitali vyenye thamani ya zaidi ya Sh. milioni 40 kutoka kwa Mkuu wa Utawala wa DKT International Tanzania, Navid Adatia vilivyotolewa na kampuni hiyo, mkoani humo juzi.
**PICHA: FRANK MONYO**

# Mwinyi akoleza dhamira kukuza utalii

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS wa Zanzibar, Dk Hussein Ali Mwinyi, amesema utalii ni moja ya vipaumbele vya serikali anayoiongoza kutokana na kuchangia asilimia 30 ya pato la taifa.

Dk. Mwinyi aliyasema hayo Ikulu, Zanzibar, alipozungumza na Waziri Mkuu wa Zamani wa Uingereza, Tony Blair, aliyefika na ujumbe wake.

Alisema Zanzibar ina utalii wa asili wa fukwe na urithi lakini kwa sasa inahitaji kwenda mbali kuboresha sekta hiyo kwa kuangalia zaidi utalii wa mikutano na michezo.

Rais Dk. Mwinyi alizitaja sekta zingine katika kukuza uchumi wa buluu kuwa ni bandari ambayo ina mchango mkubwa wa uchumi wa Zanzibar na ina mahitaji ya uwekezaji kwenye eneo hilo hasa bandari jumuishi itakayotoa huduma zote ikiwamo kuruhusu meli kubwa kushusha na kupakia vyakula, nafaka, mafuta na mahitaji mengine ya uchumi.

Kuhusu sekta ya uchukuzi kwenye uchumi wa buluu, Rais Mwinyi alisema kwa vile Zanzibar imezungukwa na Bahari, sekta hiyo pia ni muhimu, hivyo inahitaji uwekezaji mkubwa ili kuuimarisha usafiri wa majini kwa abiria na mizigo.

Pia alisema Zanzibar inahitaji uwekezaji mkubwa katika mafuta na gesi ili kuimarisha sekta ya biashara na uchumi kupitia bandari.

Alisema ushirikiano uliopo baina ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na taasisi ya Tony Blair hasa kwenye miradi mbalimbali ya huduma za jamii ikiwemo elimu na afya utaimarisha sekta zote muhimu.

Tony Blair alisifia uzuri wa kisiwa cha Zanzibar kilivyobarikiwa na kuwa na haiba na mwambao mzuri wa kumvutia kila mgeni afike kukitembelea, imejijengea sifa duniani ya kuwa na vivutio vizuri vya utalii.

Aidha, aliitaka serikali kuongeza mvuto zaidi kwa kuendelea kukipatia sifa nzuri kisiwa cha Pemba na bahati kubwa kwa Zanzibar kuwa na kisiwa kizuri kama hicho ambacho ni mfano mzuri wa kivutio cha utalii duniani.

Aliishauri serikali kuendelea kudumisha vivutio vyake vya utalii na kuendelea kuiongezea sifa Zanzibar kiutalii duniani kote.

Tony Blair ni mwanasiasa aliyehudumu nafasi ya uwaziri mkuu wa Uingereza kutoka mwaka 1997 hadi mwaka 2007.

Ni mwanasiasa wa pili kuongoza nafasi hiyo kwa muda mrefu Uingereza baada ya Margret Thatcher, aliyehudumu kwa miaka 11.

## Waziri asisitiza unafuu gharama safari za Hijja

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria , Utumishi na Utawala Bora, Haroun Ali Suleiman, amezitaka taasisi zinazosafirisha mahujaji kwenda mji mtakatifu wa Makka, Saudi Arabia, kuangalia namna ya kuwasaidia wananchi kutekeleza ibada hiyo na si kuangalia kupata faida.

Aliyasema hayo ofisini kwake, Mazizini, nje ya mji wa Zanzibar, wakati alipokabidhiwa ripoti ya Hijja ya mwaka 1444 Hijria sawa na mwaka 2023.

Haroun alisema taasisi hizo zimebeba jukumu kubwa ikiwamo kuhakikisha gharama zinazotolewa na mahujaji zinakidhi huduma zinazopatikana wakati wanapokuwa Makka kutekeleza ibada hiyo.

Alisema wananchi wengi wanaotekeleza ibada ya hijja ni wanyonge na wengi wao wamechukua muda mrefu kuweka fedha za safari ya hijja huku wengine ikiwa ni sehemu ya viinua mgongo baada ya kustaafu utumishi wa umma.

"Wakati umefika taasisi zenu ziangalie gharama halisi za hijja pamoja na huduma zinazotolewa kuona unafuu mkubwa unapatikana hatua ambayo itawawezesha watu wengi kutekeleza ibada hiyo," alisema.

Waziri huyo pia alizindua rasmi shughuli za Mfuko wa Hijja na kuitaka Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana kuanza harakati za utendaji wa mfuko huo.

Alisema uzinduzi wa mfuko wa hijja ni sehemu ya maagizo ya baraza la mapinduzi kwa ajili ya kukidhi mahitaji ya Waislamu wenye nia kufanya ibada hiyo wanapata huduma kwa njia tofauti.

"Maagizo ya Baraza la Mapinduzi chini ya Mwenyekiti wake, Rais Dk. Hussein Ali Mwinyi ,ni kuwapo kwa mfuko wa hijja ambao kazi yake ni kuratibu shughuli za ibada hiyo kwa kuangalia utaratibu wa kuwawezesha Waislamu kutekeleza ibada hiyo kwa njia tofauti," alisema.

Katibu Mtendaji wa Wakfu na Mali ya Amana, Sheikh, Abdulla Talib Abdulla, alisema ripoti hiyo inaonyesha kwa namna gani watu wengi wanazo rasilimali nyingi ambazo zinawawezesha kufanya ibada hiyo lakini hawana fedha za kutekeleza ibada. Pia alisema bado kuna changamoto nyingi kwa taasisi zinazotoa huduma kwa mahujaji ikiwamo ukosefu wa mahema wanapokuwa Minna na Arafat pamoja na kuchelewa kwa baadhi ya taarifa kwa vikundi, hivyo kusababisha kuzorota kwa baadhi ya shughuli kwa mahujaji.

Shekhe Abdulla alisema kwa mwaka huu yapo mabadiliko makubwa katika safari za ibada ya hijja Makka na baada ya kumalizika kwa ibada hiyo, tayari maandalizi ya ibada nyingine ya mwakani 2024 yanatakiwa kuanza mapema.



NASTY C AWAKUBALI MARAPA HAWA... UKURASA 14



JUMAMOSI OKTOBA 7, 2023




# DUANE "KEFFE D" DAVIS

## Alijua atakamatwa kwa mauaji?

HUYU ndiye Duane "Keffe D" Davis, ambaye kwa miaka 27 alikuwa akifurahia maisha bila kujua kwamba anafuatiliwa na polisi.

Davis (60) anatuhumiwa kupanga na kufanya mauaji ya msanii maarufu wa Hip Hop, Tupac Shakur huko Las Vegas mwaka 1996.

Kwa mara ya kwanza Davis alifikishwa mbele ya mahakama ya Nevada nchini Marekani kusomewa mashtaka yake.

Kisichofahamina na wengi kuwa polisi walikuwa wakimtafuta muuaji chini kwa chini kwa miaka 27 na mlengwa mkuu ni Davis.

Mwendesha mashtaka wa Wilaya, Steve Wolfson, ameithibitishia mahakama kuwa wana ushahidi wa kutosha na unaokubalika kisheria ili kesi hiyo isonge mbele.

Wolfson ameiambia mahakama kuwa kuna ushahidi wa kutosha wa kisheria wa kuthibitisha kwamba Davis ndiye aliyehusika na mauaji hayo.

Ameeleza changamoto inaweza kujitokeza kutokana na kesi hiyo kufunguliwa baada ya miaka 27, lakini wanaamini mfumo wa haki ya jinai utafanya kazi ipasavyo.

Davis, 60, alikamatwa Ijumaa wakati akifanya matembezi ya asubuhi karibu na nyumba yake katika kitongoji cha Henderson na saa chache alifikishwa katika Mahakama ya Wilaya ya Clark ikimshtaki kwa mauaji.

Duane Davis alikiri hadharani kuhusika kwake katika mauaji hayo kwenye mahojiano na baadae alizungumza kwenye simulizi yake ya 2019 iliyoitwa "Compton Street Legend."

"Kuna jambo moja ambalo ni la uhakika unapoishi maisha ya majambazi tayari unajua kuwa vitu ulivyoweka vitarudi; haujui jinsi au lini, lakini hakuna shaka kuwa vinakuja." alisema

Maoni hayo ya Davis yalifufua uchunguzi wa polisi ambao ulisababisha kufunguliwa mashtaka.

BASI SAWA

## Marafiki Music Festival ilivyowasha moto jukwaa

TAMASHA la muziki la Marafiki limeanza kwa kishindo kwa wasanii waliofanikiwa kupanda jukwaani kutoa burudani iliyowapagawisha mashabiki waliohudhuria.

Tamasha hilo la siku tano linafanyika katika viwanja vya Makumbusho mkoani Dar es Salaam na kuwahusisha wasanii kutoka mataifa mbalimbali duniani.

Wasanii waliofanikiwa kukonga nyoyo za watu usiku wa kuamkia jana ni Salma Munde na Msafiri Zawose kutoka Tanzania, kundi la Sun XaExperiment la Afrika Kusini, Amos Lovinz kutoka Uganda, Kadilida na RDJ Kwaro.

Wanamuziki hao walitumbuiza kwa nyimbo zenye maadhi mbalimbli na kuwafanya waliohudhuria kufurahia burudani hiyo.



## Starshine ampongeza Diamond



Msanii wa Bongo Fleva anayefanya vizuri na wimbo Mi Aliento, Starshine, amesema ubunifu na akili nyingi za Diamond ndio sababu ya kutajwa katika tuzo za MTV EMA mwaka huu.

Diamond Platnumz alitangazwa kuwa ni msanii pekee wa Tanzania kuwania tuzo kubwa duniani za MTV Europe Music Awards 2023 katika kipengele cha Best African Act.

Starshine, amesema Diamond atabaki kuwa mfano wa kuigwa kwa jinsi anavyotumia ubunifu na akili nyingi kusukuma mziki wake.



## SALMA MUNDE AONYESHA YEYE MALKIA WA JAZZ


Mwanamuziki pekee wa kike wa muziki wa Jazz, Salma Munde, amesema anapambana kuona Watanzania wanaanza kuupenda muziki huo unaonekana kama mgeni kwao.

Akizungumza na BT mara baada ya kutumbuiza tamasha la muziki la Marafiki, Munde amesema amefurahi kuona watu wamempokea vizuri na wameonyesha dalili ya kumuunga mkono kwa kile anachokifanya.

"Nilipopanda jukwaani niliona watu wakifurahia kutokana na mtindo wangu wa uimbaji na muziki, najua hawajazoea aina hii ya muziki lakini kuna kila dalili ya kuniunga mkono kwa jinsi walivyonipokea," amesema Munde.

Amesema tamasha hilo la Marafiki limezidi kumuonyesha njia ya mafanikio hasa kwa kumpa heshima ya kuwa wa kwanza kupanda jukwaani.





## Huddah hawapendi chawa

MPAMBAJI wa video za wanamuziki Afrika Mashariki, Huddah Monroe amewajia juu watu wenye tabia za kujipendekeza na kutumia matukio ya vifo kama njia ya kujipatia umaarufu.

Amesema kuna baadhi ya watu wanatumia vifo vya watu kama sehemu ya kutafuta kiki, na amewashauri kutafuta aina nyingine ya kupata umaarufu badala ya kutumia vifo vya watu wengine.

"Baadhi ya watu huwadhihaki wafu kana kwamba wataendelea kuwa vijana milele na kamwe hawatakufa. Ni haki ya kupita kwetu sote. Jinyenyekezeni. Ni zamu kwa zamu," amesema.

## MA-QUEEN WAKALI PICHA ZA KIDOSI

**Na Adam Fungamwango**

KAMA unakumbuka miaka ya 1980 hadi 1990 kulikuwa na filamu nyingi za Kihindi ambazo wakati huo vijana wa mjini walipenda kuziita 'picha za Kidosi.'

Ndiyo kipindi ambacho kulikuwa na makumbi makubwa, au majumba ya kuonyesha filamu hizo kama Drive Inn Cinema, Avalon, Empress, Cameo, Empire, New Chox, na maeneo mengine mbalimbali. Hiyo ilikuwa ni miaka ya 1980.

Ilipofika miaka ya 1990, televisheni zilipoanza kuingia, hata mitaani sasa watu walikuwa wanaonyesha filamu hizo. Watoto wa mjini wakaviita vibanda umiza.

Filamu mbalimbali za kihindi zilitikisa sana. Leo sitawataja mastaa wa picha hizo, bali ni wale washiriki wao wa kike katika filamu hizo.

Hawa mara nyingi hucheza kama wenza au wapenzi wa mastarlingi katika filamu husika, maarufu kama makwini.

**Hema Malini**

Huyu ndiye kwini wa filamu za Kihindi anayetambulika zaidi na maarufu kuliko wengine.

Hema Malini ndiye aliyeongoza njia za wanawake wengine kupita alipopita yeye.

Amecheza kama kwini katika filamu nyingi sana za kihindi, akijipatia sifa na tuzo nyingi.

Alizaliwa India, Oktoba 16, 1948 na huwezi kuorodhesha filamu zake alizocheza Bollywood kwa sababu ni nyingi mno.

Aliolewa na staa mwingine wa picha za Kihindi, Dharmendra ambaye ni baba wa watoto wawili wacheza filamu maarufu,  Sunny Deol na Bobby Deol ambao waliwakuta.

Yeye mwenyewe alifanikiwa kupata watoto wawili wa kike na staa huyo ambao ni Esha Deol na Ahana Deol.

**Kimi Katkar**

Kwini huyu anajulikana pia kwa jina la Ruby Shetty. Ni kwa sababu ya filamu iliyomtambulisha zaidi na kumpa sifa, Adventures of Tarzan ya mwaka 1985 ambayo alitumia jina hilo.

Ndiye alikuwa kwini wa filamu hiyo kwa kumpenda kijana ambaye alionekana kama nusu binadamu na nusu mnyama.

**Shilpa Shetty**

Wale wanaopenda picha za Kidosi watakubaliana na mimi kuwa mwanadada huyu aliyecheza filamu nyingi za Kihindi ni mmoja kati ya makwini ambao mbali ya kuwa mwigizaji, amejaaliwa urembo kupindukia. Baazigar ndiye filamu iliyomtambulisha.

**Karisma Kapoor**

Huyu ni mmoja wa makwini maarufu waliocheza filamu nyingi za Kihindi. Alizaliwa 1974, baba yake alikuwa mwigizaji Randhir Kapoor na ana dada yake ambaye pia ni mcheza sinema Kareena Kapoor.

**Kajol Devgan**

Ni mmoja kati ya makwini wa filamu warembo kuwahi kutokea kwenye taifa la India, ambaye angeweza kabisa kuwania hata ulimbwende na kutwaa urembo wa dunia. Moja ya filamu nyingi zilizompatia umaarufu ni 'Kuch Kuch Hota Hai.'



FILAMU

## Niachie Mke Wangu: Mke anauma

**Na Adam Fungamwango**

HIKI ni kisa cha kusikitisha cha jamaa mmoja ambaye angeweza kumtafuta msichana mmoja na kuwa mpenzi wake, badala yake akaanza uhusiano wa kimapenzi na mke wa mtu.

Kisa hiki kipo kwenye filamu iitwayo 'Niachie Mke Wangu.' Mambo haya yapo kwenye jamii na yamekuwa yakisababisha madhila, watoto kuteseka kwa kukosa walezi ya baba na mama ambao wanalazimika kuachana.

Bado kuna madhara mengi kwani wengine wanachukua hatua mkononi kama vile kuua, kujiua, lakini pia msongo wa mawazo.

Ngoi ni mwanamume ambaye alimkuta msichana mmoja aitwaye Tatu na mdogo wake Amina wakiwa katika hali mbaya. Baada ya kufiwa na wazazi wao wakawa hawana nyuma wala mbele, wanahangaika mitaa wasijue pa kula wala kwa kulala.

Akawachukua na kuwapeleka nyumbani kwake. Baadaye akafunga ndoa na Tatu.

Miaka michache tu ya ndoa, Tatu anabadilika kitabia. Anaingia kwenye mahusiano na mwanamume mwingine aitwaye Mudi.

Hata hivyo hakuna anachofanya zaidi ya mapenzi tu, kwani yeye ndiye anayemgharamia mchepuko wake kwa chakula, nguo na malazi. Pesa anatoa kwa mumewe.

Kikubwa zaidi ni kwamba hata heshima kwa mumewe inapungua kiasi kwamba Ngoi anaanza kuhisi kuna kitu.

Kuna siku anarejea nyumbani mapema na kumkuta mkewe njiani ameshika 'hotipoti' la chakula anapeleka kwa bwana.

Hali hii ilimfanya Ngoi kutokuwa na raha kabisa. Amina, pamoja na kumkanya dada yake Tatu, lakini na yeye akawa anaambulia matusi.

Siku isiyo na jina Ngoi aliwafuma laivu, mkewe na Mudi ingawa wao hawakumuoa.

Kesho yake akaenda nyumbani kwa Mudi kumkanya amuache mkewe, lakini na yeye aliambulia vitisho.


Hatima yake ndoa ilivunjika, mke akaondoka nyumbani na akaenda kwa Mudi. Lakini mwanaume huyo hana lolote, hali ya maisha ikaanza kuwa mbaya.

Mwisho wa siku Mudi akataka kumbaka Amina. Hali hiyo ikamkera sana Tatu.

Baada ya kupata shutuma kila kona, wazazi wake, rafiki, mpaka watu mitaani, akinyooshewa vidole kila anapopita, akaamua kwenda kumuomba msamaha Ngoi na kumsihi amchukue mkewe.

Ngoi akakataa msamaha wake na kumwambia kwa sasa yeye anaangalia mbele, hawezi kumrudia, aendelee naye tu na anaanza upya.





# Burna Boy, Rema, Aseke watamba MTV Europe

WANAMUZIKI wa kiafrika Burna Boy, Rema na Asake majina yao yanatamba katika tuzo za muziki za MTV Europe baada ya kujitokeza katika vipengeleze zaidi ya kimoja.

Katika kifurushi kipya cha Best Afribeats, ambacho kimeanzishwa kwa mara ya kwanza mwaka huu wasanii watakaowania ni Aya Nakamura , Asake, Arya Starr, Burna Boy, Davido na Rema wote kutoka Nigeria.

Wakati huo huo, wimbo wa pamoja wa Rema na Selena Gomez 'Calm Down' uliteuliwa katika vipengele vya 'Wimbo Bora' na 'Best Collaboration'.

Asake, Burna Boy, diva wa Cameroon, Libianca, nyota wa Tanzania, Diamond Platnumz na Tyler ICU wa Afrika Kusini waliteuliwa katika kipengele cha 'Best African Act'.

Burna Boy pia aliteuliwa katika kipengele cha Best Live Performer akiwa na Beyoncé, Ed Sheeran, Taylor Swift na The Weeknd.



## Nasty C awakubali marapa hawa...

MSANII wa Hip hop kutoka Afrika Kusini, Nsikayesizwe David Junior Ngcobo, maarufu kama Nasty C, amewasifia wanamuziki wa Nigeria kwa kufanya kazi kwa ubunifu kiasi ambacho kimemfanya kuiga.

Amewataja marapa kama Olomide, Phyno, Sakordie, AKA na Nyovest ni wanamuziki wenye nguvu na ubunifu wa hali ya juu kila wanapotoa nyimbo zao.

Kijana huyo mwenye umri wa miaka 26 alifichua hilo katika mahojiano ya podcast na Afrozons.

## Wafurahia Naira Marley kukamatwa

MASHABIKI wa muziki nchini Nigeria wamepongeza hatua ya jeshi la polisi kumkamata na kumshikilia nyota wa Afrobeats Naira Marley katika uchunguzi unaondelea wa kifo cha mwanamuziki Mohbad.

Taarifa ya polisi wa Jimbo la Lagos kwenye mtandao wa kijamii wa X (zamani wa Twitter) ilisema wamemkamata msanii huyo mara baada ya kurejea kutoka Marekani.

"Azeez Fashola almaarufu Naira Marley amekamatwa kwa ajili ya mahojiano", aliandika Benjamin Hundeyin, msemaji wa Polisi wa Jimbo la Lagos.





## Linda asahau alichofanyiwa Lagos

MWIGIZAJI wa Nollywood Linda Osifo amesema alipata wakati mgumu kuchagua maisha ya Nigeria au Canada ambako aliishi kwa muda mrefu.

Msanii huyo mkongwe katika filamu amesema pamoja na changamoto alizokumbana nazo baada ya kuhamia Nigeria, imemfanya kuimarika na kukuza kipaji chake cha uigizaji.


|Amesema hapo mwanzo haikuwa rahisi kumudu maisha ya jiji la Lagos, kwani alijaribu kuandaa matamasha mbalimbali lakini kutokana na ugeni wake hakupata kitu na kufanya kuvunjika moyo.

## Staa 'Harry Potter' afariki dunia

STAA wa filammu kutoka Ireland, Michael Gambon, anayejulikana sana kama Profesa Dumbledore katika filamu za Harry Potter, amefariki dunia.

Muigizaji huyo alifariki baada ya kuugua ugonjwa wa nimonia, kulingana na familia yake.

CNN, ilifichua katika taarifa yake kwamba mwigizaji huyo aliaga dunia kwa amani akiwa amezungukwa na familia yake akiwa hospitalini.



# Wapewa siku 60 kusalimisha silaha

Na Hamida Kamchalla, TANGA

JESHI la Polisi mkoani Tanga, limetoa siku 60 kwa watu wote wanaomiliki silaha kinyume cha sheria kuzisalimisha kabla ya Novemba 30, mwaka huu.

Kwa mujibu wa Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Tanga, Kamishna Msaidizi (ACP) Almachius Mchunguzi, kwa muda ambao umetolewa ni vyema kila aliye na silaha anayoimiliki kinyume cha sheria, aisalimishe ili hatua isichukuliwe dhidi yake.

Agizo hilo linashajihishwa na msamaha wa kutoshtakiwa kwa wale wote watakaozisalimisha silaha hizo kwa mujibu wa Kifungu cha 64 cha Sheria ya Udhibiti wa Silaha na Risasi ya Mwaka 2015, Sura ya 223.

"Niwatake wananchi katika mkoa wa Tanga, wilaya zote, hata kama ndugu yako alikuwa anamiliki na amefariki dunia, inapaswa kuletwa polisi na kusalimishwa. Pia mtu kama anayo silaha na anajua kuwa anaimiliki isivyo halali, aisalimishe kituo cha polisi au katika ofisi za watendaji hawatashtakiwa.

"Katika kipindi hiki ambacho Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi (Hamad Masauni), ametoa msamaha kwa wanaosalimisha silaha kwa hiari, watakaokaidi niwatangazie kabisa kuwa kutakuwa na msako mkali usiokoma. Wako watu wanatengeneza silaha kama magobole halafu wanayatumia kufanyia uhalifu," alisema.

Kamanda Muchunguzi alisema kumekuwa na kesi za mara kwa mara kuhusu wanaojihusisha na utengenezaji wa magobole katika maeneo ya vijijini, jambo ambalo limekuwa likiendelea bila watu hao kuwa na woga.

Agosti 30, mwaka huu, Msemaji wa Jeshi hilo, Kamisha Mwandamizi Msaidizi (SACP) David Misime, alisema kufanya hivyo ni kudhibiti uzagaaji wa silaha haramu kama ilivyokuwa makubaliano ya 2018 ya udhibiti wa silaha hizo.

# Waziri apiga stop ujenzi kituo cha mafuta

Na Mwandishi Wetu, MOSHI

WAZIRI wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Jerry Silaa, amesimamisha ujenzi wa kituo cha mafuta kinachojengwa na mwanasiasa mmoja katikati ya Mji wa Moshi, mkoani Kilimanjaro.

Silaa ameelekeza kuanzia sasa ujenzi huo kusimama hadi ruhusa itakapotolewa ya kuendeleza ujenzi huo.

Waziri huyo alifikia uamuzi huo juzi, alipofanya ziara yake ya kwanza katika Manispaa ya Moshi, kuangalia matumizi ya ardhi na kukutana na wataalam wa ardhi kutoka wilaya sita za mkoa huo.

Kwa mujibu wa Silaa, sheria iliyotumika kutoa eneo hilo inaonekana kutokuwa sawa.

"Nikiuliza kuhusu kikao mlichokaa mwaka 2018 mkaamua vituo vya mafuta vitoke mita za mraba 3,000 kwenda 4,000 mlikuwa mmezingatia jambo gani? Tunapata shida.

"Kutokana na wizara kufanya mageuzi makubwa hata wale waliofanya mambo haya ya ukiukwaji, watafanyiwa mageuzi. Naagiza ujenzi wa kituo hicho usitishwe hadi pale ruhusa ya kuendelea na ujenzi itakapotolewa," alisema.

Awali, akitoa ufafanuzi kuhusu kibali hicho, Richard Emily, ambaye ni Ofisa Mipango Miji wa Manispaa ya Moshi, alisema mfanyabiashara huyo ambaye pia ni mwanasiasa, alikidhi vigezo kulingana na sheria iliyopo kwa sasa.

"Eneo hili linapatikana katika michoro ya mipango miji na mwaka 2022, mmiliki alibadili matumizi ya kiwanja hicho kwenda kituo kidogo cha uuzaji wa mafuta na alikubaliwa kufanya mabadiliko hayo baada ya kupewa kibali na wizara pamoja na Mkurugenzi wa Manispaa," alisema Emily.



Katibu Mkuu mpya wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Dayosisi ya Kaskazini Mashariki, Mwalimu Julius Madiga akitia saini kitabu cha wageni baada ya kuripoti katika ofisi ya Askofu wa Dayosisi hiyo, Msafiri Mbilu (kulia), wilayani Lushoto, mkoani Tanga hivi karibuni. Katibu huyo, anatarajiwa kuingizwa kazini rasmi kesho Jumapili, wilayani Handeni. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# Wananchi wakumbwa na hofu ya mafuriko

Na Tumaini Mafie, ARUMERU

HOFU ya kukumbwa na mafuriko kwa wakazi wa Kata ya Oltrumet iliyoko Mamlaka ya Mji Mdogo wa Ngaramtoni, wilaya ya Arumeru mkoani Arusha, imewaibua wananchi wake, hivyo kuiomba serikali kuwajengea miundombinu ya maji, hasa mifereji inayoruhusu maji kuondoka kwenye eneo hilo.

Wananchi hao wameanza kupaza sauti zao ili seerikali iwanusuru na mafuriko endapo yatatokea baada ya Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA), kutahadharisha juu ya mvua El-Nino ilizotabiri kwamba zitashuhudiwa kuanzia Oktoba hadi Desemba, mwaka huu.

Kwa nyakati tofauti jana, wakazi wa kata hiyo, waliieleza Nipashe kuwa wako katika hofu kubwa hususani kipindi hiki ambacho mvua zimeanza kunyesha.

Aprili, mwaka huu, mvua za masika zilisababisha uharibifu mkubwa wa mali na mazao ya wanachi katika kata za Oltrumet, Oloirien, Sambasha, Olmotonyi na Kimnyaki.

Zawadi Laizer, mkazi wa Kiushini-Seuri, kata ya Oltrumet, alisema hofu yao inatokana na mazingira wanayoishi kwamba ni lazima yataathiriwa na kuharibiwa vibaya na mafuriko kama mvua za El-Nino zitanyesha kwa kipindi kilichotajwa kama ilivyotabiriwa.

Alisema mvua zilizoanza kunyesha juzi, wanasita kuwaruhusu watoto kwenda shuleni, wakihofia endapo mvua zitazidi, watoto hawatarudi nyumbani.

William Lukumay, alisema: "TMA imetangaza wananchi tuchukue tahadhari lakini sisi hata kulala ndani tunaogopa. Tukiona kumefunga tunachanganyikiwa.

Hapa mvua imenyesha wenzetu wanafurahia lakini sisi tunawaza tutanusurika? "alihoji Lukumay.

Katibu wa Chama cha Mapinduzi (CCM) wa Kata hiyo, Naftali Michael, alisema wananchi wanakosa imani na chama hicho, kwa kutoboreshewa miundombinu na kuwekewa makinga maji.

"Wananchi wamekichukia chama kwa namna ambavyo wanateseka na mafuriko. Mvua zimeanza watu hawana amani, kulala ndani ni hofu, mawasiliano ya barabara yalikatika tangu mwanzoni mwa mwaka huu. Wananchi hawana barabara ya kupita, serikali itukumbuke hatuna cha kuwaeleza watu," alisema.

Diwani wa Kata hiyo, Joseph Tinayo, amejitetea kwamba amekuwa akieleza kero hiyo katika Baraza la Madiwani la Halmashauri ya Arusha, huku akikosa kupatiwa majibu kuhusu ufumbuzi wa tatizo lao.

"Tunamwomba, Mkuu wa Mkoa na Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan, watusaidie hii kero ya barabara kwa wakazi wa Seuri.

"Hatuna haja ya kuendelea kuitwa Madiwani, kwa kuwa wananchi wanatutukana wanaona kama hatufikishi kero zao halmashauri, lakini tunazisemea kila siku. Tumechoka na iko siku tutaachana na uwakilishi huu wa Udiwani," alisema Tinayo

TULIKOTOKA, TULIPO & TUNAKOKWENDA

# Unawakumbuka wavuta kiko na mbwembwe zao?

## -Walipenda kukaa kwa mikogo, sharubu ndefu na kujiamini

**Na Adam Fungamwango**

SI rahisi kwa sasa kukuta hata watu wazima wanavuta kiko kama ilivyokuwa zamani, achilia mbali vijana.

Inawezekana ikawa fasheni hiyo kwa sasa haipo, au hawa watu wa sasa hawana watu ambao wanaweza kuwa vioo au 'roll model', au kuwashawishi kufanya hivyo.

Waliobaki wanamalizia kuvuta kwa sasa ni wale wazee wa zamani enzi za mkoloni.

Kiko ni nini? Ni mtemba au chombo kinachomwezesha mtu kuvuta moshi wa tumbaku, au kitu kingine chenye uraibu unaovutwa kama sigara. Kiko hutengenezwa kama mrija hivi na mbele unaunganika na mzunguko ambao ukubwa wake na ulivyo unafanana sana na kikombe cha kahawa, kama picha zinavyoonyesha.

Kwa wale watu wazima watamkumbuka mwanasiasa mmoja machachari, aliyewahi kuwa mbunge wa Bukoba, na Waziri wa Kazi na Maendeleo ya Vijana, Sebastian Kinyondo (marehemu).

Mheshimiwa huyu alama yake kubwa ni kuvuta kiko au mtemba na alikuwa akionekana nao popote pale, labda tu ndani ya bunge. Kiko ndiyo ilikuwa alama yake kubwa kiasi cha kupewa jina la utani, mzee wa mitemba. Uvutaji wa kiko ulianza zamani sana na uliletwa na wakoloni.

Wale wavutaji wa kiko enzi hizo walivutiwa sana na wakoloni wa Kijerumani na Kiingereza ambao ndiyo hasa waliowaambukiza babu zetu kuvuta kiko au mtemba.

Kama ilivyo kawaida, wanapokuwa wakoloni ni lazima wataleta utamaduni wao na wanaotawaliwa wataingiwa na kitu kinachoitwa kasumba, yaani kupenda vitu vya wanaowatawala.

Awali Waafrika hawakuwa na kitu kinaitwa kiko, badala yake walikuwa wakivuta aina fulani ya kitu kinaitwa gozo.



Hii inafanana sana na sigara, lakini tumbaku yake inawekwa na kufungwa kwenye majani yaliyokauka.

Mtu anapovuta hili gozo linakuwa na harufu kali. Wale waliokuwa wakisafiri kwenye treni za TRC miaka ya 1970 hadi 1980 mwishoni watakumbuka harufu hii ilikuwa inapatikana sana kwenye mabehewa ya daraja la tatu. Lakini wakati huo ilikuwa inavutwa na watu wa hali ya chini tena, siyo waliosoma.

Kwa sababu wazungu ambao ni wakoloni walichukuliwa kwamba ni watu wa daraja ya juu na watawala kwa hiyo kila walichokuwa wakifanya kilichuliwa kuwa ni bora zaidi, na hata wenyewe walianza kuwaaminisha wanaowatawala kuwa kila kitu wanachofanya hakina maana na ni ushamba.

Kunywa uji wa mihogo ni ushamba na mtu wa maana anatakiwa anywe chai na mikate.

Dawa za mitishamba zikaitwa ni za kishenzi, badala yake zikaletwa za Kizungu. Waafrika walikuwa wanapiga mswaki kwa aina fulani ya miti maalum ambayo ina dawa asili ndani yake.

Lakini jamaa wakaja na miswaki yao ya plastiki na dawa za meno za kiwandani na hadi leo hii akionekana mtu anapiga mswaki kwa mti, huyo ni mshamba.

Tukirudi kwenye mada yetu ya kiko ni kwamba Wabongo walioanza kuvuta ni wale waliosomeshwa na wakoloni, wakaelimika na kuwa makarani na kazi zingine ambazo wakati huo zilionekana za juu kuliko za ukulima na ufugaji.

Nao wakaanza kujiona bora kuliko wenzao, wakaanza kuchukua utamaduni wa kizungu kwa kuanza kuvuta kiko badala ya gozo.

Wakajiambukiza na hata tabia zao. Ndiyo maana kipindi hicho ukimuona mtu anayevuta kiko wa Kiafrika atakuwa tofauti na wazee wenzake, au watu wengine.

Kwanza atakuwa msomi, halafu wavuta kiko wote ni kama wamezaliwa baba mmoja na mama mmoja, tabia zao zilikuwa zinafanana.

Licha ya kwamba wanakuwa wasomi, walikuwa ni watu wa kujiamini sana. Wana msimamo, hawana wasiwasi, na wakivuta mitemba yao wanakuwa na mbwembwe kwa kupenda kukaa kiupande upande, wakiwa na mikogo na dharau kwa mbali.

Pia wavuta kiko wengi wao walikuwa na masharubu marefu, au ndevu nyingi. Walikuwa wakiwaiga wazungu.

Kwa sasa utamaduni wa uvutaji kiko unatoweka kwa kasi na unaweza kukaa hata mwaka mzima usione mtu yeyote anayevuta.

Hata watu wazima sasa hawavuti, vijana ndiyo kabisa. Wengi wao wanavuta sigara tu. Kwa sababu kile kizazi kilichochukua utamaduni wa kizungu moja kwa moja kutoka kwa wakoloni kinaishia.

Wakati naweka mada hii kwenye mtandao, kuna mdau mmoja akaulizia wapi wanapouza kiko kwa sababu babu yake anamsumbua sana.

"Jamani natafuta kiko (mtemba wa kuvutia tumbaku). Babu yangu anasema atanipa laana nisipompelekea. Nimejitahidi kumweleza madhara ya tumbaku lakini kasema ameanza kuvuta tangu zama hizo. Kiko chake kimevunjika na hakifai tena anasema alikinunua wakati wa mkoloni. Nimepita madukani hakuna, nimeona bora nije hapa, hata kama babu yako alikuachia urithi we niuzie nikamfurahishe babu yangu."



Aliyewahi kuwa mbunge wa Bukoba, na Waziri wa Kazi na Maendeleo ya Vijana miaka ya nyuma, hayati Sebastian Kinyondo alikuwa mvutaji maarufu wa kiko kiasi cha kupewa jina la utani, mzee wa mitemba.


Kuna mmoja alimjibu ameshawahi kuziona zikiuzwa kwenye maduka fulani jijini Arusha na kupeana mawasiliano ili waweze kukamilisha hilo.

"Kuna mzee mmoja Mkufunzi pale NIT Dar es Salaam (amestaafu) na hata tumbaku havuti tena. Sasa sema unazo shilingi ngapi nichome mafuta sasa hivi? Najua atakuwa navyo kadhaa kwenye makumbusho yake," mwingine alimjibu.

"Duh Mkuu hiyo kitu imenikumbusha mbali sana, kulikuwa na mzee mmoja jirani yetu, miaka hiyo ya nyuma, alikuwa akifanya Relwe, (TRC), alikuwa na sharubu za haja na kutwa yupo na kiko yake mdomoni, alikuwa akijiita Mdachi au Mjerumani." Akaandika mdau mwingine.

**Tuma meseji 0716 350534**







# Mfungwa ashinda tuzo ya Nobel

**OSLO,** NORWAY

MWANAHARAKATI wa haki za wanawake nchini Iran, Narges Mohammadi ambaye amefungwa jela, ametangazwa kuwa mshindi wa Tuzo ya Amani ya Nobel 2023.

Mwenyekiti wa Kamati ya Tuzo ya Amani ya Nobel Berit Reiss-Andersen, alimtangaza Narges Mohammadi, ametunukiwa kutokana na ujasiri wake wa kupigania haki na kupinga ukandamizaji wa wanawake nchini mwake.

Mohammadi ni miongoni mwa wanaharakati wanawake wa Iran ambao wamekuwa mstari wa mbele kupigania haki nchini humo baada ya kisa kilichohusisha kifo cha Mahsa Amini kilichotokea mikononi mwa polisi.

Jumla ya watu 351 ikiwa ni pamoja na mashirika mbalimbali ni miongoni mwa walioteuliwa kushindania tuzo hiyo mwaka huu.

**DW**

# Watoto milioni 41 wakosa makazi

**NEWYORK,** MAREKANI

MAJANGA yanayotokana na hali mbaya ya hewa yamesababisha watoto milioni 43.1 kupoteza makazi kati ya 2016 hadi 2021.

Kulingana na ripoti ya Shirika la Umoja wa Mataifa la kuwahudumia Watoto UNICEF, ilisema majanga hayo yalichochewa na mabadiliko ya tabia nchi ni pamoja na mafuriko, ukame, vimbunga na moto wa misituni.

Kulingana na ripoti hiyo, mafuriko na vimbunga vilisababisha asilimia 95 ya makazi kupotea.

Laura Healy, mtafiti mwenza wa ripoti hiyo aliliambia shirika la habari la AFP kwamba ilikadiriwa kuwa takriban watoto 20,000 walilazimika kuyakimbia makazi yao kila siku.

Hali hiyo inaonyesha jinsi watoto walioathiriwa wako katika hatari ya kukumbwa na matatizo zaidi, kama vile kutengwa na wazazi wao au kuwa waathirika wa walanguzi wa watoto.

Wataalamu wametahadharisha kuwa katika miaka 30 ijayo, mafuriko yanaweza kusababisha watoto milioni 96 kuhama makazi yao.

**DW**

# Russia yafanikiwa jaribio kombora hatari la nyuklia

**MOSCOW,** RUSSIA

NCHI ya Russia imetangaza kufanya jaribio la mwisho lenye mafanikio la kombora hatari la nyuklia.

Rais Vladimir Putin ametoa tangazo hilo siku chache baada ya msemaji wake kukataa majaribio ya silaha hiyo inayojulikana kama Burevestnik, yaliyokuwa yanakaribia.

Silaha iliyofanyiwa majaribio, ilitangazwa kwa mara ya kwanza mnamo 2018, na ilisifiwa kuwa na uwezo wa kuruka umbali wa masafa yasiyo na ukomo.

Hata hivyo, kulikuwa na taarifa kidogo zinazojulikana kuhusu uwezo wake na kuna ripoti kwamba majaribio ya awali yalifeli.

Ukurasa wa Rais Putin haujathibitisha na hakuna taarifa zozote kutoka kwa wizara ya ulinzi ya Russia kuelezea tukio hilo.

Picha za satelaiti zilizosambazwa mwezi uliopita zilionyesha kuwa Russia ilikuwa imejenga vifaa vipya hivi karibuni katika eneo la mbali la kisiwa cha Aktiki kulikofanyika majaribio ya nyuklia ya Umoja wa Soviet miaka ya nyuma.

Baadhi ya picha hizo zilionyesha kazi za ujenzi zikiendelea eneo la Novaya Zemlya, katika kisiwa kilicho kaskazini mwa Bahari ya Barents.

"Sasa tumemaliza kazi ya aina za kisasa za silaha za kimkakati ambazo nimezizungumzia na nilitangaza miaka michache iliyopita," Putin aliambia mkutano katika eneo la mapumziko la Bahari Nyeusi, Alhamisi ya wiki hii na kutangazwa moja kwa moja kwenye runinga ya serikali.

"Jaribio la mwisho lililofanikiwa limefanyika Burevestnik, kombora la kimataifa linalotumia nguvu za nyuklia." aliongeza kiongozi huyo.

Kombora hilo, lililopewa jina la Skyfall na Nato, linasemekana kuendeshwa na kinu cha nyuklia, ambacho kinatakiwa kuwashwa baada ya viboreshaji vya roketi za mafuta kulirusha angani.

Lakini gazeti la New York Times lilinukuu kundi la kampeni ya kudhibiti silaha, Nuclear Threat Initiative, likisema kwamba majaribio 13 ya awali ya mfumo huo kati ya 2017 na 2019 yote hayakufaulu.

Rais Putin pia aliwaambia wasikilizaji wake kwamba kazi ilikuwa karibu kukamilika kwa kombora la masafa marefu, linaloitwa Sarmat.

Alisema Russia haina mpango wa kubadilisha sera yake ya nyuklia inayoweka wazi mazingira ambayo majeshi yake yanaweza kutumia silaha za aina hiyo.

Aliongeza kuwa uwepo wa serikali ya Russia hauko chini ya tishio na hakuna mtu mwenye akili timamu na kumbukumbu safi ambaye atafikiria kutekeleza shambulio la nyuklia dhidi yake.

**BBC**



Wafanyakazi wa dharula wakizima moto baada ya shambulizi la Russia katika mji wa Kharkiv mashariki mwa Ukraine jana. **PICHA: REUTERS**

# Kombora laua watu 51 Ukraine

**KYIV,** UKRAINE

RUSSIA imefanya mashambulizi ya makombora na kuua watu 51 katika kijiji cha Hroza, kusini-mashariki mwa mji wa Kharkiv nchini Ukraine.

Taarifa kutoka maofisa wa serikali ilisema watu waliofariki walikuwa wakihudhuria mkesha wa mazishi ya mkazi wa eneo hilo.

Wizara ya ulinzi ya Ukraine ilisema hakukuwa na maeneo ya kijeshi yaliyolengwa ni raia pekee.

Mkuu wa mkoa wa Kharkiv, Oleh Synyehubov alielezea shambulizi hilo kama moja ya uhalifu wa umwagaji damu uliowahi kutokea katika eneo hilo. Alithibitisha kuwa watu waliofariki ni wakazi wa kijiji hicho, na kwamba shambulio hilo liliua asilimia 20 ya wakazi wake.

"Moja ya tano ya kijiji hiki wamefariki katika shambulio moja la kigaidi," alisema kwenye televisheni ya taifa.

Waziri wa Mambo ya Ndani wa Ukraine, Ihor Klymenko alisema kila kaya iliathirika katika kijiji hicho.

"Kutoka kila familia, kutoka kila kaya, kulikuwa na watu waliofariki" alisisitiza

Mtandao wa Interfax Ukraine uliripoti kuwa mazishi hayo yalikuwa ya mwanajeshi wa Ukraine.

Miongoni mwa waliofariki ni mjane, mtoto na mkwe wa mwanajeshi huyo.

Hapo awali mwanajeshi huyo alikuwa amezikwa huko Dnipro, lakini jamaa zake walisema walitaka kumzika tena kijijini kwao.

Rais wa Ukraine Volodymyr Zelensky, alisema kitendo hicho hakiwezi kuitwa cha kinyama kwa sababu kitakuwa tusi kwa wanyama.

Aliishutumu Russia kwa kulenga kijiji hicho kimakusudi wakati watu walikusanyika kwa ajili ya ibada ya kumbukumbu.

**DW**

MATANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTELEWA NA CHETI



**STEPHEN LWEGANWA KEZILAHABI** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S3470/0116** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **ABBEY SEKONDARI** mwaka 2020. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/DAR/ILA/21153/2023.**

## CHANGE OF NAME BY DEED POLL

**REGISTRATION OF DOCUMENTS ACT (CAP 117 R.E 2019)**

**BY THIS DEED I,** the undersigned **VAILETH VEDASTO KIBASILA** of P.O Box 116, Morogoro and a citizen of United Republic Of Tanzania by birth **DO HEREBY:**

**1) FOR AND BEHALF OF MY SELF,** I absolutely renounce, relinquish and abandon the use of the former names of **VAOLETH KIBASILA VEDASTO** in place thereof do maintain from the date of birth and herein state the name of **VAILETH VEDASTO KIBASILA** and so that I may, hereafter be called, known and distinguished not by the names **VAOLETH KIBASILA VEDASTO** but by the name of **VAILETH VEDASTO KIBASILA.** For the purpose of evidencing that my determination I declare that I shall in all time records, deeds and writings, in all actions and in all occasions whatsoever use, sign the name of **VAILETH VEDASTO KIBASILA** as my name in place of the names of **VAOLETH KIBASILA VEDAST**O so relinquished as aforesaid to the intent that I may hereafter be known not by the aforesaid former names, but by the maintained name of **VAILETH VEDASTO KIBASILA.**

2) I hereby authorize and request all persons and authorities to designate and address me in the name of **VAILETH VEDASTO KIBASILA** on this day and in the manner herein stated.

3) **IN WITNESS** whereof I have hereunto subscribed my new name of **VAILETH VEDASTO KIBASILA** and have affixed my signature the day and year herein written.



SIGNED and DELIVERED in Morogoro
by the said VAILETH VEDASTO KIBASILA
who is personally known to me
this 2nd day of October, 2023 — Deponent

BEFORE ME:
Name: IGNAS SETI FUNGE
Address: P.O. Box 9, Mzumbe
Signature:
Qualification: Advocate & Commissioner for Oaths

## KUPOTEA KWA KADI YA GUTA

**BWANA DAMAS KOSMA FUNGO WA IRINGA** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GUTA YENYE USAJILI **MC 382 CUG.** YOYOTE ATAEFANIKIWA KUIONA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI KILICHOPO KARIBU NAE POLISI TAARIFA **PHQ/IRI/IRI/1710/2023**

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**IDDY SALUM SELEMANI NGALLA** Anatangaza kupotelewa na kadi ya **PIKIPIKI (FEKON)** yenye namba za usajili **T 832 CXN,** jina kwenye kadi ni **TANZANIA CHINA TRADE AND TOURISM DEVELOPMENT LT,**Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo cha polisi **PHQ/MOR/MOR/3575/2023.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**AYUBU MUHIDINI KIMARO** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 745 DFK TOYOTA COASTER.** Chassis No. **HZB360001160.** Engine No. **IHZEAA1160.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi kilichopo karibu. Taarifa ya Polisi: **PHQ/ARU/ARU/3821/2023.**

## KUPOTEA KWA CHETI



**ABEDINEGO CHRISTOPHA NTUKULA** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S.0341/0086** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia SANGU SEKONDARI mwaka 2020. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **MBE/MBE/RB/165826/2023.**

## KUPOTEA KWA CHETI



**ANGOLILE STEPHANO** anatangaza kupotea kwa cheti cha **CHUO KIKUU CHA TEOFILO KISANJI** kilichotolewa mwaka 2013. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **MBY/RB/597/2019.**

**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA YA NZEGA**

**MAOMBI YA ARDHI NA. 15 YA MWAKA 2023**

**ROSE MANGILIMA....................................MWOMBAJI**

**DHIDI YA**

**HOSEA PETER .................................MJIBU MAOMBI**

**KUITWA SHAURINI**

Mjibu maombi **BW. HOSEA PETER** popote ulipo unafahamishwa kwamba **BIBI ROSE MANGILIMA** amefungua maombi ya Ardhi Na. 15/2023 Katika baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya lililopo Nzega. Shauri husika limepangwa kusikilizwa tarehe 17/10/2023. Saa 2:30 asubuhi. Hivyo unatakiwa kuleta utetezi wako ndani ya siku 7kuanzia tarehe ya kutolewa tangazo hili. vielelezo vyote nya kesi vinapatikana katika Masjala ya wazi Baraza la Ardhi na Nyumba (W)- Nzega
Unafahamishwa kwamba usipohudhuria maombi husika yatasikilizwa bila ya wewe kuwepo/kutoa utetezi wako na kutolewa hukumu.
Imetolewa na kutiwa saini na Muhuri wa Baraza hili leo tarehe 04/10/2023

V. A.LING'WENTU
MWENYEKITI
BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA (W)
NZEGA

**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA**

**WILAYA YA KINONDONI MWANANYAMALA**

**SHAURI LA MADAI NAMBARI 405 LA 2019**

**ABDALLAH SAANANE.............MUOMBAJI/WAOMBAJI**

**DHIDI YA**

**1) MADUHU UYUBU**
**2) MUSSA SAID.......................MDAIWA/WADAIWA**

**WITO KUITWA SHAURINI**

**1) MADUHU UYUBU**
**2) MUSSA SAID............................POPOTE ULIPO/MLIPO**

**ABDALLAH SAANANE** amefungua shauri mbele ya Baraza la Ardhi na Nyumba lililopo Kinondoni (Mwananyamala). Shauri husika limepangwa kutajwa/kusikilizwa tarehe 11/10/2023 saa 3:00 asubuhi mbele ya Mh. J.W. SILLAS. Hivyo unaamriwa kuhudhuria mbele ya Baraza siku hiyo bila kukosa.

Imetolewa na kutiwa saini na Mhuri wa Baraza hii leo tarehe 25 Mwezi wa 09 Mwaka 2023.

MWENYEKITI
BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA (W) KINONDONI

**FORM 58**
**GENERAL CITATION**
**(Rule 75)**
**IN THE HIGH COURT OF TANZANIA**
**(DAR ES SALAAM DISTRICT REGISTRY)**
**AT DAR ES SALAAM**
**MISC. CIVIL APPLICATION NO. 418 OF 2023**
**(Originating from the probate and Administration Cause No. 37 OF 2015)**
**IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE WILLIAM ESTOMIH URONU**
**AND**
**IN THE MATTER OF PETITION FOR GRANT OF LETTERS OF ADMINISTRATION IN RESPECT OF UNADMINISTERED ASSESTS**
**BY**
**HELLEN WILLIAM URONU............................THE PETITION**

All persons claiming to have any interest in the estate of the above named WILLIAM ESTOMIH URONU deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they fit before the grant of probate (or letters of administration) is made to the above named HELLEN WILLIAM URONU petitioner.
Objections to the grant should be filed or before the 18th day of October, 2023.
Dated at Dar es salaam this 02 day of 10, 2023.

Deputy Registrar

**KIBAIGWA AUCTION MART**
**P.O.BOX 20, DODOMA**

**TANGAZO LA MNADA WA HADHARA KIBAIGWA AUCTION MART,**

KWA IDHINI NILIYOPEWA NA KAMPUNI YA IMARISHA MAISHA FINANCIAL SERVICES LTD. TUTAUZA MAGARI MAWILI 1. MALI YA BARAKA NYANG'ANYI MALELA YENYE NAMBA ZA USAJILI T390 DCN AINA YA SUBARU IMPREZA 2. MALI YA SOSPETER ISAYA CHIUYO YENYE NAMBA ZA USAJILI T828 CUS. AINA YA SUZUKI CARRY. MNADA UTAFANYIKA TAREHE 06/11/2023 MAENEO YA NYERERE SQUARE SAA 10:00 ASUBUHI

**KWA MAWASILIANO ZAIDI PIGA NO. 0688 729841**

## MNADA WA HADHARA

Kutakuwepo na mnada wa hadhara wa kuuza dhamana za wadaiwa sugu. Mnada utaendeshwa na madalali tajwa hapo chini kwa idhini ya **Tujijenge Tanzania Financial Service Ltd** kama ilivyotangazwa gazetini:-

| Mdhamini/ Mdaiwa | Dhamana/ Mahali ilipo | Tarehe ya mnada/ Dalali |
|---|---|---|
| Nisile Boaz Mwakajumba | Nyumba- Majohe Kichangani DSM | 25. 10.2023 Rapitech Solurions Ltd |
| Haji Jamadin Chitonya | Nyumba– Yombo Vituka Barabara ya Mwinyi DSM | 27.10.2023 Rapitech Solutions Ltd |
| Matiku Mgaya Masabi | Nyumba- Mtaa Kilungule (Buza) -DSM | 20.10.2023 Rapitech Solutions Ltd |
| Gregory Isdory Wenceslaus | Nyumba- Kimara Michungwani -DSM | 13.10.2023 White Miracles (T) Ltd |
| Hilda Archady Kikatuka | Nyumba -Mbugani Kishiri - Mwanza | 28.10.2023 Mase International Ltd |
| Bahati Maseko Godfrey | Nyumba – Mtaa Ndofe Kishiri - Mwanza | 28.10 .2023 Mase International Ltd |
| Nassoro Salum Kibichi | Nyumba – Nzasa 'B' Mbagala –DSM | 27.10.2023 SEPCO Debt Collection |
| Elizabeth Leonard Ogugu | Business chattels – Tawi la Gongo la mboto -DSM | GEMSUD Investment Ltd – 20.10.2023 |

**Masharti Mengine:**
Minada yote itafanyika mahali dhamana zilipo kuanzia saa nne asubuhi. Mteja atalipa 25% siku ya mnada, 75% atalipa ndani ya siku 14, akishindwa kulipa 25% iliyolipwa hairudishwi. Gharama za kuona, kukagua, kuhamisha umiliki, kumtoa mdaiwa/ mpangaji ni juu ya mnunuzi.

**Mawasiliano piga: MASE – 0784717164/ 0743885084 White Miracles-0782359900; SEPCO- 0715683777 RAPITECH-0628866132; GEMSUD- 0652113262**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**JEROME AMBROSE MWASSE** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 401 BMC** yenye Chassis No. **KDH2055000677.** Engine No. **2KD1311842.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi kilichopo karibu. Taarifa ya Polisi: **PHQ/ARU/ARU/3783/2023**

**TANZANIA HOME ECONOMIC ASSOCIATION [TAHEA] WANATANGAZA**

KUPOTELEWA NA CHETI CHA KUFUATA **"CERTIFICATE OF COMPLIANCE"** NO: 1732. YEYOTE ATAEFANIKIWA KUKIONA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI KILICHOPO KARIBU NAE, POLISI TAARIFA **IRI/IRI/RB/69861/2022.**

**OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI INDUSTIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710. E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**

Kwa Habari Motomoto usikose

Gazeti lako la Nipashe kila siku

*Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi*

*Kwa Bei Poa*

*Tupigie 0745 700 710.*

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji

THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# HADITHI

MBWA mmoja wa jirani wa maeneo ya Kinondoni Msisiri, alionekana kuvutiwa na kiroba kilichotupwa upenuni mwa nyumba moja. Ni moja kati ya viroba ambavyo hutupwa usiku au alfajiri na vijana wanaokusanya taka kwenye nyumba za watu na kupewa ujira kidogo. Wao badala ya kwenda kutafuta maeneo ya kutupa, hupita vichochoroni na kama hajaonekana anautupa mzigo na kuendelea na safari yake. Ilitokea kwenye nyumba moja huko, na mbwa huyo alipouvuta, viungo vya mwili wa binadamu vilianguka. Majirani wa kwanza kuona walipiga kelele na watu wakajazana. Akinamama wakiangua vilio. Viungo vilihifadhiwa kwa kufunikwa. Polisi walianza msako. Kwa kuanzia tu wakaanza kuwakamata wazoa taka na waokota chupa za kwenda kuuza, wote wa maeneo hayo na jirani wanaofahamika tayari kwa mahojiano na uchunguzi, wakihisiwa kuwa huenda mmoja wao au zaidi kuhusika na mauaji. Ni maiti ya nani? Na Muuaji ni nani? Fuatilia mwanzo hadi mwisho kujua mkasa mzima ulivyokuwa.

## MAITI KWENYE KIROBA-29

**Na Adam Fungamwango : (0716 350534)**

"Ina maana Charton amemuua mkewe kwa kudanganywa tu na huyo mwanamke anayeitwa Rukia?"

"Ndiyo hivyo ili mke aachwe aolewe yeye kwa sababu alikuwa anataka hivyo tangu mwanzo."

"Enhee nimesahau, pia mwezi mmoja tu kabla ya kuletewa hiyo picha, mwanamke alinunua gauni linalofanana sana na lile alilovaa. Mume alipoiona akajua ni picha mpya, wajihi wa mkewe na lile gauni. Nasikia Charton kwa ukatili wake hata hakumwambia kitu chochote mkewe. Nadhani labda angekaa naye na kumuuliza mkewe angeweza kumuonyesha vitu mbalimbali kwenye hiyo picha vinavyoonyesha ni ya zamani, lakini mwenyewe akapanga mpango huo wa kumuua bila kumwambia kitu. Kwanza alituma watu kumsaka Barton kimya kimya hawakumuona, ndiyo akafanya mauaji yake kwa mkewe."

"Sasa mpenzi kwa nini hili usiende kulisema polisi ili jamaa akakamatwa?" Eddy alichombeza.

"Weee! Unamjua yule jamaa! Kuna baadhi ya maafande wako mikononi mwake, ana pesa mtu kama mimi si naweza kufagiliwa mbali, nikafa na mimi maiti yangu ikatupwa baharini ndugu zangu wakakosa hata mwili wa kuuzika!" Akajibu na kumfanya Eddy kuangua kicheko.

Kwa maelezo hayo tayari Eddy alipata mtuhumiwa mwingine ambaye ni Rukia. Yeye ndiyo chanzo cha mauaji. Kumshawishi Charton kuamini mkewe ni mzinzi kwa ajili ya kiu yake ya mapenzi.

******************************

"Haloo Afande Frank?" Eddy akaita.

""Ndiyo mkubwa niambie."

"Mnaendeleaje huko?"

"Sisi tupo vizuri, sijui nyinyi huko?

"Tuko vizuri, na leo nataka nikuambie kuwa leo tumemaliza kila kitu."

"Eeeee, usiniambie bwana."

"Tumempata mwingine wa ziada, huku ndiye chanzo cha yote."

"Enhee, hebu nipe hiyo habari."

"Ni hivi mimi nimeshakamilisha kazi na napenda niwasilishe ifuatavyo.

Mboneka Fisimaji aachie mara moja baada ya kumkamata mtu mmoja anaitwa Charton Antony na mpenzi wake Rukia. Hao waunganishwe na Tinga Patauli kwenye kesi ya mauaji."




**Wakati Nancy akijua amepata mpenzi mpya baada ya kutemwa na Charton, Eddy alimtumia kwa ajili ya**

"Okay, nitawatuma vijana wangu waifanye hiyo kazi, kusema kweli leo nitalala usingizi mnono, maana kazi itakuwa imekamilika." Inspekta Frank alionyesha furaha isiyo kifani.

"Halafu napenda kuuliza, kila kitu, vielelezo viko tayari kwa ajili ya kuwapeleka mahakamani?"

"Na ndiyo maana nilichelewa kukupatieni majina na muendelezo kwa sababu nilikuwa kwenye uchunguzi wa kina na nimekusanya kila kitu ambacho kila mmoja anahusika nacho, kesho mchana ufike ofisini kwangu, nitakukabidhi kila kitu kwa ajili ya kukamilisha ufunguaji wa kesi."

"Ahsante sana Eddy Kamal, upelelezi wako umeliheshimisha taifa, nadhani tukishatangaza wananchi watafurahi sana, maana wamekuwa wakilifuatilia sana hili suala." Inspekta Frank akakata simu.

Alibaki na furaha kwa sababu alijua atapanda cheo. Hilo aliahidiwa mapema na mabosi wake.

Ni yeye ndiye aliyetoa wazi kwa Jeshi la Polisi kumtumia mpelelezi Eddy Kamal kuchunguza mauaji ya mwanamke mmoja mrembo aitwaye Tessy. Yalikuwa mauaji ya kinyama ambayo wauaji walimkatakata kama nyama ya bichani kitu kilichozua mihemko na hasira kutoka kwa wananchi.

Wakaitaka serikali kumkamata muuaji au wauaji hao. Awali waliotiwa mbaroni ni waokota chupa na wabebataka wa maeneo ya Kinondoni Msufini.

Ni kwa sababu mabaki wa maiti walikutwa kwenye kiroba, hivyo ikadhaniwa kuwa baadhi yao ndiyo waliotekeleza mauaji hayo na kuutelekeza kwenye moja ya nyumba za wakazi wa huko kabla mbwa kunusa harufu na kuchakura.

Alipotoa kiungo kimoja kutoka kwenye kiroba, ndipo watu walipojua kuwa kilikuwa kiroba kilichotiwa viungo vya maiti baada ya kukatwakatwa.

Eddy aliongeza na Inspekta Frank na kumpa taarifa hiyo siku moja tu baada ya kuachana na mpenzi wake 'feki' mpya, Nancy.

Wakati Nancy akijua amepata mpenzi mpya baada ya kutemwa na Charton, Eddy alimtumia kwa ajili ya upelelezi na si kitu kingine.

Hata hivyo alijua maumivu yatakayompata msichana huyo akigundua hilo. Hakutaka kumpema mapema. Atakuwa naye kwa muda ili kumpa faraja. Ikibidi hata mwaka, na ataachana naye kwa namna ambayo haitampa maumivu Nancy.

****************************

Ndani ya ofisi ya Eddy Kamal. Alikuwa amekaa kwenye kiti chake maalum na kompyuta yake mbele.

Alikuwa amepokea mgeni maalum, Inspekta Frank. Lengo lilikuwa ni kumpa mrejesho mzima wa kazi aliyoifanya mwanzo hadi mwisho. Pia kukabidhiwa nyaraka ambazo ni ushahidi dhidi ya watuhumiwa wote waliofanya uhalifu huo.

Baada ya salamu na utani wa hapa na pale, Eddy alikusanya vielelezo vyote ambavyo aliona vinafaa kupelekwa mahakamani. Hata hivyo alichotoa ni kopi ya vielelezo, huku nyaraka halisi akibaki nazo mwenyewe.

"Bwana Frank, kilichotokea kwenye kesi hii ambacho mimi nimekipeleleza ni kwamba, kuna dada mmoja anaitwa Rukia. Alisoma na marehemu Tessy. Charton aliwafahamu na kutokea kumpenda Tessy kiasi cha kumuoa. Lakini ndani ya moyo wake Rukia yeye alimpenda Charton. Ikakaa akilini mwake kuwa ipo siku ataisambaratisha ndoa na Charton ataingia mikononi mwake.

Katika pitapita zake akafanikiwa kupata picha ya mwanaume mmoja aliyepiga na Tessy miaka mingi sana nyuma. Mwanaume huyo ni kweli alikuwa mpenzi wa Tessy kabla ya kukutana na Charton. Na yeye mwenyewe Rukia anamfahamu. Mtu huyu anaitwa Barton. Kwa sasa nasikia anaishi nchini Uingereza.

Rukia aliipeleka kwa makusudi na kumuonyesha Charton ambaye naye bila kuhoji au kutafakari akaamini kuwa mkewe anamsaliti.

Ukweli ni kwamba picha ile ilipigwa zamani, Charton akadanganywa kuwa ni mpya.

Na kilichomuaminisha zaidi kuwa ilikuwa mpya ni wajihi wa mkewe. Alimkuta akiwa mwembamba sana kutokana na maisha yaliyokuwa anaishi kipindi hicho.

Sasa ile picha afande alionekana amenawiri kama ilivyo sasa kwa hiyo jamaa akajua haikupigwa muda mrefu sana. Kumbe Tessy kabla maisha hayajampiga kwa kuachana na mwanaume wake Barton alikuwa mrembo kama alivyokuwa kabla ya kuuawa.

**ITAENDELEA JUMAMOSI**

# SINGIDA FG YASEMA MTIBWA SUGAR IMEWAPA KIPIMO KIZURI KWA SIMBA

**Na Saada Akida**

KOCHA Msaidizi wa Singida Fountain Gate FC, Thambo Senong amesema mechi yao iliyopita dhidi ya Mtibwa Sugar imewapa kipimo kizuri kuelekea mchezo wao wa kesho dhidi ya Simba.

Singida FG juzi ilipata ushindi wa kwanza tangu pazia la ligi hiyo kufunguliwa baada ya kuifunga Mtibwa Sugar bao 1-0, uwanja wa Manungu, Tuliani mkoani Morogoro. Katika michezo minne iliyocheza Singida FG imeshinda mchezo mmoja, imetoa sare mbili na imepoteza mchezo mmoja ikikusanya alama tano na inashika nafasi ya nane kwenye msimamo wa Ligi kuu.

Akizungumza na Nipashe jana, Thambo alisema mechi na Mtibwa Sugar walicheza vizuri na wametumia mchezo huo huo kujiandaa na mchezo wao wa kesho Jumapili dhidi ya Simba.

Alisema wameridhishwa na kiwango cha wachezaji walichokionyesha kwenye mchezo uliopita na wanaamini wataendeleza kile walichokifanya kwenye mchezo wa kesho.

"Tunasahau matokeo ya mechi iliyopita dhidi ya Mtibwa, tunaangalia mbele sasa, mchezo wetu ujao ni dhidi ya Simba nyumbani, tunahitaji kupata matokeo chanya kulingana na ubora wa wapinzani wetu," alisema Thambo.

Aliongeza wamefanyia kazi mapungufu madogo waliyoyaona kwenye mchezo wao dhidi ya Mtibwa Sugar ikiwemo umakini wa wachezaji wake hasa safu ya ushambuliaji kutumia nafasi zinazopatikana kupata matokeo mazuri.

"Haitakuwa mechi rahisi, tunaenda kucheza kwa nidhamu ya hali ya juu kuhakikisha hatufanyi makosa ambayo yatatuadhibu kwa kupoteza nyumbani, Simba ni timu kubwa na ina wachezaji wazuri hivyo lazima tujipange vizuri kuwakabili " alisema Kocha huyo msaidizi.




Mkurugenzi wa Kitengo cha Huduma kwa Wateja wa Airtel Tanzania, Adriana Lyamba ( wa tatu kushoto) na Katibu Tawala Msaidizi, Viwanda, Biashara na Uwekezaji wa Mkoa wa Dodoma, Mwajabu Nyamkomora (kushoto) wakiserebuka pamoja na wahudhuriaji wengine wakati kikundi cha ngoma za asili kikitoa burudani katika Viwanja vya Nyerere, jijini Dodoma, ikiwa ni sehemu ya shamrashamra za maadhimisho ya Wiki ya Huduma kwa Wateja, mjini humo jana. **PICHA: MPIGA PICHA WETU**

# Kundemba, Mlandege hapatoshi Zanzibar leo

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

MAHASIMU wawili katika Ligi Kuu ya Zanzibar, Kundemba FC na Mlandege FC wanakutana leo katika muendelezo wa Ligi hiyo ikiwa mzunguko wa tano huku mchezo huo ukitarajiwa kuwa na upinzani kubwa.

Mchezo huo ambao umepewa jina la 'Majirani Derby' ni mara ya Pili timu hizo zinakutana tangu Kundemba ilipopanda daraja na kucheza Ligi kuu ya Zanzibar misimu miwili iliyopita.

Mara ya Mwisho timu hizo zilikutana Msimu uliopita ambapo katika mzunguko wa kwanza Kundemba ililala bao 1-0 na mzunguko wa pili ililipiza kisasi kwa kushinda kwa idadi kama hiyo.

Akizungumza na Nipashe jana Kocha wa Kundemba FC ,Ali Vua alisema wamejipanga kuhakikisha wanapata alama tatu katika mchezo huo.

Alisema ingawa mchezo huo utakuwa mgumu sio tu kwa kuwa ni Majirani Derby lakini pia kulingana na matokeo ya michezo iliyopita kwa timu hizo.

Alisema Kundemba FC ilipoteza kwa kufungwa michezo miwili mfululizo ya Ligi Kuu ya Zanzibar huku majirani zao nao walitoka sare michezo miwili mfululizo jambo ambalo kila timu inahitaji kupata alama tatu.

Alisema kuelekea mchezo huo ambao mashabiki wa timu zote wanahitaji timu zao kupata alama tatu hivyo kwao watafanya kila jitihada ili kuhakikisha alama tatu zinapatikana.

"Tunaenda kucheza mchezo mgumu wenye kuhitaji matokeo ya alama tatu, mchezo ambao pia umebeba hisia za mashabiki zetu kuona tunawafunga wapinzani wetu ambao ni majirani zetu, hivyo lazima wachezaji wajitume kwa hali ya juu kuhakikisha tunatimiza lengo letu" alisema Vua.

Kundemba FC ipo nafasi ya tisa ikiwa na alama nne wakati wapinzani wao Mlandege FC ipo nafasi ya sita ikiwa na alama sita katika msimamo wa Ligi kuu ya Zanzibar inayodhaminiwa na Benki ya PBZ.

# Mabondia 108 kushiriki pambano la Dk Samia

**Na Shufaa Lyimo**

MABONDIA 108 wa ngumi za kulipwa nchini leo wanatarajia kushiriki katika pambano la ngumi la 'Dk. Samia Open Boxing Tournament' linalotarajiwa kuanza leo viwanja vya Tanganyika Packers, jijini Dar es Salaam.

Mabondia hao jana walipima uzito kwenye viwanja vya shule ya Kimataifa Getrude Rwakatare tayari kwa mapambano hayo yatakayofikia tamati Oktoba 14 siku ya kumbukizi ya kifo cha Mwalimu Julius Nyerere.

Mashindano hayo yameandaliwa na Ofisi ya Diwani kata ya Kawe, chini ya Diwani Mutta Rwakatare kwa kushirikiana na taasisi ya ' Bega kwa Bega na Mama Samia Suluhu Hassan'.

Akizungumza na gazeti hili jana, Mratibu wa pambano hilo, Salum Viduka alisema miongoni mwa mapambano hayo kutakuwa pia na mapambano matatu ya wanawake.

" Baada ya kugundua kuna vijana wengi wanaofanya mazoezi ya mchezo wa ngumi ila hawapati mechi (mapambano) tukaona ni vyema kuanzisha mashindano haya, mabondia wapate fursa ya kuonyesha uwezo wao", alisema Viduka.

Alisema mashindano yana lengo la kusaka, kuibua na kuendeleza vipaji vilivyo jificha kupitia 'Gym' wanazocheza.

"Tutasherehekea siku ya kumbukizi ya kifo cha muasisi wa taifa letu Mwalimu Julius Kambarage Nyerere siku ya Oktoba 14 mwaka huu ambayo ndiyo kilele cha mashindano haya, "alisema Viduka.

Wakati huo huo Makamu wa Rais wa Kamisheni ya ngumi za kulipwa nchini (TPBRC) Nasoro Chuma alisema wanamuunga mkono diwani wa Kawe Ruta Rwakatare kwa kuamua kuanzisha jambo hilo.

Alisema sasa hivi wametoa kipaumbile kwa mapromota kuandaa mapambano kwa kupunguza ada ya kuandaa mapambano.

"Sasa hivi mapromota wanatoa sh. 50, 000 tofauti na hapo awali walikuwa wanatoa 100, 000, ki ukweli Rwakatare amefanya jambo ambalo litazidi kuinua mchezo huu "alisema Chuma.

Aliwataka watanzania wajitokeze kwa wingi kushuhudia vijana wakionesha vipaji vyao kwenye viwanja hivyo vya Tanganyika Packers.

# Raga Dar yaandaa darasa la saratani

**Na Shufaa Lyimo**

CHAMA cha Raga Tanzania (TRU)kimeandaa mashindano ya wanawake ya mchezo huo yatakayofanyika Oktoba 28, mwaka huu katika eneo la Ukonga, Dar es Salaam.

Lengo la mashindano hayo ni kuwapa wachezaji wanawake elimu ya kuufahamu na kuuelewa ugonjwa wa saratani ya matiti.

Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake wa TRU, Fatma El Kindly alisema maandalizi kuelekea mashindano hayo yatakayoshirikisha timu mbalimbali za mkoa wa Dar es Salaam yanaendelea vyema.

El Kindly alisema siku hiyo kutakuwa na mchezo mmoja ambao utawakutanisha wenyeji Ukonga Queens dhidi ya Weedo Warriors.

"Tunafanya mazungumzo na baadhi ya taasisi kwa ajili ya kutusaidia kutoa elimu kwa wanawake na wanafunzi wakike namna ya kujikinga na ugonjwa wa saratani ya matiti, tunawaomba wadau kujitokeza siku hiyo ili tufikie malengo," alisema El kindly.

## ZISIKUPITE

### CHELSEA YAKOMAA NA TONEY
MATUMIZI makubwa ya Chelsea yanatazamiwa kuendelea Januari huku klabu hiyo ikimlenga mshambuliaji wa Napoli mwenye umri wa miaka 24, Victor Osimhen na mshambuliaji wa Brentford ya England, Ivan Toney mwenye umri wa miaka 27. (***Guardian***)

### CHELSEA YATAKA MIL 500
KLABU ya Chelsea pia inatafuta mkopo wa pauni milioni 500 ili kufadhili usajili huo baada ya kutumia pauni bilioni moja katika kipindi cha madirisha matatu ya uhamisho. (***Sun)***

### ARSENAL NA PHILLIPS
KLABU ya Arsenal itamgeukia kiungo wa kati wa Manchester City na England, Kalvin Phillips mwenye umri wa miaka 27 Januari huku washikabunduki hao wakipania kuimarisha safu yao ya kati. (***Fichajes***)

### YAMAL KUSAINI MPYA
WINGA wa Barcelona mwenye umri wa miaka 16 raia wa Hispania, Lamine Yamal anatazamiwa kusaini mkataba mpya wa miaka mitatu na klabu hiyo, ambao una kipengele cha kuachiliwa kwa pauni bilioni 1. (***Fabrizio Romano***)

### NEWCASTLE YAMTAKA ANDERSON
KLABU ya Newcastle inamfuatilia mlinzi wa Crystal Palace raia wa Denmark, Joachim Andersen kwa nia ya kumnunua mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 27 Januari. (***Football Insider)***

### ANSU FATI KUUZWA
BARCELONA iko tayari kumuuza mshambuliaji wa Hispania, Ansu Fati msimu ujao wa joto baada ya mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 20 kumaliza muda wake wa mkopo Brighton. (***Sport***)

### MESSI AMTAKA MODRIC
LIONEL Messi ameitaka Inter Miami kumsajili kiungo wa kati wa Real Madrid na Croatia, Luka Modric mwenye umri wa miaka 38. (***Cadena Ser***)

### ALEXANDER MSHAHARA JUU
LIVERPOOL imekubaliana kimsingi na beki wa England, Trent Alexander-Arnold kwa mkataba mpya, ambao utamfanya mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 24 kulipwa zaidi ya pauni 200,000 kwa wiki, pamoja na bonasi. (***Football Insider)***

### MOSCARDO AWINDWA BARCA
BARCELONA imeanza mazungumzo na Corinthians kwa ajili ya kumnunua kiungo wa kati wa Brazil mwenye umri wa miaka 18, Gabriel Moscardo huku wakitarajia kuipiku Chelsea kwenye usajili wake. ***(Sport via Goal)***

### RABIOT MKATABA MPYA
KLABU ya Juventus inatumaini la kumpa mkataba mpya kiungo wa kati wa Ufaransa, Adrien Rabiot mwenye umri wa miaka 28, baada ya kukataa kuhamia Manchester United msimu wa joto. (***Tuttosport***)

### TAPSOBA AWANIWA
KLABU ya Tottenham inataka kumsajili beki wa Bayern Leverkusen mwenye umri wa miaka 24 raia wa Burkina Faso, Edmond Tapsoba Januari (***Fichajes***)

### RIGGE AGOMBEWA
KIUNGO wa kati wa timu ya taifa ya vijana ya England, Dan Rigge mwenye wa miaka 17 anatazamiwa kusaini mkataba mpya wa muda mrefu katika klabu ya West Ham, licha ya klabu nne za Ligi Kuu ya England na mbili za LaLiga zikihitaji huduma yake. (***Fabrizio Romano***)

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# MESSI KURUDI BARCELONA

**MIAMI,** Marekani

### ●●●Kwa ajili ya kumuaga pindi atakapotundika daluga rasmi...

NAHODHA na Mshambuliaji wa Argentina, Lionel Messi ameahidiwa kufanyiwa jambo la kipekee ili kuagwa rasmi ndani ya Barcelona pindi atakapofikia mwisho wa maisha yake ya soka.

Jorge Mas, ambaye anamiliki Klabu ya Inter Miami sambamba na David Beckham, alisema amempa gwiji huyo ahadi yake kwamba atafanya kila linalowezekana kukamilisha jambo hilo kwa staa huyo anayeitumikia klabu hiyo hivi sasa.

**"Messi alipoondoka Barcelona hakuweza kuiaga klabu yake ambayo ilimkaribisha akiwa mtoto, nadhani mazingira hayakuwa yale ambayo Lionel alitaka," alisema kiongozi huyo na kuongeza.**

"Nilimpa (Messi) ahadi yangu kwamba nitafanya kila niwezalo katika miaka ijayo ili apate fursa ya kuwaaga mashabiki wake huko Barcelona.

"Inter Miami itakwenda (kwa Barcelona) au tutakuwa na aina fulani ya mechi."

Messi alidumu ndani ya Barcelona kwa kipindi cha takribani miaka 20 baada ya kujiunga na klabu hiyo akiwa na miaka 13, akaondoka mwaka 2021 na kutua PSG, kabla ya 2023 kujiunga na Inter Miami.

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!

SUPA JACKPOT KWA 1000/- 1,159,5

MECHI KALI

GEITA GOLD FC
VERSUS
YOUNG AFRICANS

1 | 6.90
X | 4.34
2 | 1.40

tigo pesa SportPesa

WASHINDI WA MAOKOTO Deilee!

1. Joseph Bilali - 0652 077 XXX
2. Rehema Issa - 0654 594 XXX
3. Fikiri Madenge - 0673 395 XXX
4. Nice Mmbugu - 0675 299 XXX
5. Kareem Kamota - 0675 366 XXX
6. Firoz Dhalla - 0713 786 XXX
7. Matokeo Bakecha - 0714 138 XXX
8. Selemani Kuteya - 0714 523 XXX
9. Joshua Kampauni - 0715 859 XXX
10. Shabani Ally - 0717 833 XXX

20,000/= KWA KILA MMOJA

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#

GBT:0249 HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA: 0764115588, 0677115588 0685115588
18+
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa



# BEN CHILWELL NJE HADI DESEMBA 2023

**LONDON,** England

BEKI wa Chelsea, Ben Chilwell atakuwa nje ya uwanja hadi Desemba 2023 kufuatia jeraha la misuli ya paja.

Beki huyo wa kushoto alipata tatizo hilo katika dakika za mwisho za ushindi wa Chelsea wa bao 1-0 dhidi ya Brighton katika Kombe la Carabao Jumatano iliyopita.

Kwa mujibu wa gazeti la Telegraph, Chilwell huenda akawa nje kwa angalau majuma manane kutokana na jeraha hilo.

Imeripotiwa pia kuwa anaweza kuwa nje ya dimba kwa muda mrefu zaidi kulingana na mwenendo wa jeraha, mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 26 aliondolewa kwenye kikosi cha England kilichoshiriki Kombe la Dunia kipindi cha kiangazi mwaka jana kutokana na tatizo la misuli ya paja.

Lakini alirejea kucheza Februari mwaka huu na kurudi katika nafasi yake kwenye kikosi cha Gareth Southgate.

Chilwell alianza katika kikosi cha kwanza England ilipocheza mechi za kufuzu Kombe la Euro 2024 dhidi ya Ukraine mwezi uliopita lakini atakosa mechi zilizobaki za Kundi C.

Beki huyo ambaye ni nahodha chaguo la pili Chelsea amecheza mechi moja ya Ligi Kuu England na hakujumuishwa katika kikosi kilichocheza dhidi ya Fulham, ambapo The Blues ilishinda 2-0 kupitia mabao ya kipindi cha kwanza ya Mykhailo Mudryk na Armando Broja.

Kocha wa Chelsea Mauricio Pochettino alifafanua kuhusu hali ya Chilwell kabla ya mechi hiyo ya London Dabi alisema: "Nadhani ni habari mbaya. Kwa alivyoniambia daktari sio njema."

# Materazzi amlipua Lukaku



**MILAN,** Italia

ALIYEKUWA Beki wa Inter Milan, Marco Materazzi, amebainisha kwamba, anataka kufahamu kwa nini Romelu Lukaku hakurejea klabuni hapo na kuamua kwenda AS Roma kwa mkopo akitokea Chelsea.

Materazzi amebainisha kwamba, Lukaku msimu uliopita alifanya mazungumzo ya kujiunga na Juventus wakati akiwa bado ni mchezaji wa Inter Milan, kitu ambacho ni kama usaliti.

"Ni aibu. Nataka kufahamu nia yake ilikuwa nini," alisema Materazzi.

Alipoulizwa ni vipi atakaribishwa Inter katika mchezo wa Serie A utakaofanyika Oktoba 29, mwaka huu huko San Siro, Materazzi alisema: "Anafahamu, nadhani itakuwa vibaya. Ni kawaida kwamba alisaliti mara moja, akasamehewa, kisha akasaliti mara ya pili."

Lukaku amewahi kuitumikia Inter Milan vipindi viwili tofauti, awali ilikuwa 2019 hadi 2021alipotua mara ya kwanza akitokea Manchester United, kisha msimu wa 2022-2023 akicheza kwa mkopo akitokea Chelsea.

HABARI MICHEZO

574,731/-

# KMC YAWACHIMBA MKWARA WABABE WA YANGA SC

Na Adam Fungamwango

LICHA ya wapinzani wao kufanikiwa kupata ushindi kwenye mchezo wao uliopita dhidi ya mabingwa watetezi, Yanga, KMC imeionya Ihefu SC kuwa haitokuwa rahisi kutoka na ushindi mwingine leo hii kwenye Uwanja wa Uhuru, Dar es Salaam watakapokutana kwenye mzunguko wa tano wa ligi kuu Tanzania Bara.

KMC imesema na wao wanataka kuendeleza moto wao wa ushindi mfululizo baada ya kuifunga Geita Gold mabao 2-1 katika mechi iliyochezwa Jumamosi iliyopita kwenye Uwanja wa Nyankumbu, Geita.

Kocha Mkuu wa timu hiyo Abdihamid Moallin amesema hawatoingia uwanjani kwa kuihofia Ihefu kwa sababu wameifunga Yanga, bali wanataka kucheza na kupata ushindi na kuendeleza kile walichokifanya ugenini wiki iliyopita.

"Kwanza kabisa napenda kushukuru kwa viongozi na kamati iliyonichagua kuwa kocha bora wa mwezi Septemba na mchezaji wangu Waziri Junior kuwa mchezaji bora wa mwezi, yale tuliyoyafanya mwezi uliopita tunataka kuyafanya pia mwezi huu wa Oktoba, kuna mchezaji wangu hapa Awesu Awesu huwezi kujua anaweza kuwa mchezaji bora wa mwezi huu, tuzo hizi zimetufanya, kutushawishi na kuwa deni kwa ajili ya kufanya vyema zaidi ya hapa.

Lakini hapa tuna mchezo wetu tutakaokwenda kucheza na Ihefu, malengo yetu ni pointi tatu kesho, Mungu akipenda," alisema kocha huyo.

Aidha, mchezaji wa timu hiyo Awesu Awesu amesema wachezaji wenzake wote wanatambua kuwa wanakwenda kucheza mchezo mgumu, hivyo wamejiandaa kwa utimamu wa mwili na kiakili pia.

Kocha Mkuu wa Ihefu, Zuberi Katwila alisema mechi hiyo itaamuliwa kifundi zaidi na kwao baada ya kuifunga Yanga wana deni lingine kupata muendelezo.

"Tumejiandaa na mechi hii tukijua tunacheza ugenini, mchezo utaamuliwa kiufundi zaidi kwa sababu ukitoka kushinda pambano kama lile dhidi ya Yanga, basi mpinzani anayekuja mbele yako anajiandaa vizuri zaidi, inabidi tufanye kazi ya ziada na wachezaji wanalijua hilo," alisema.




Rais wa Chama cha mchezo wa Gofu kwa Wanawake Tanzania (TLGU),Queen Siraki,akipiga mpira wakati wa mashindano ya mchezo huo ya NCBA Golf Series, yaliyofanyika katika viwanja vya Gymkhana jijini Dar es Salaam hivi karibuni. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## Yanga SC kumaliza hasira kwa Geita

INATOKA UK 24

wala kufanyia kazi makosa yaliyojitokeza kwenye viwanja vya mazoezi, na pia napenda kubadilisha wachezaji wangu katika mechi mbalimbali kwa sababu wanaocheza nao pia ni binadamu, wana matatizo, wana familia kama ilivyo kwa kila mtu, hivyo wanaweza kufanya makosa," alisema Gamondi.

Kwa upande wake, Kocha wa Geita Gold, Hemed Suleiman 'Moroco' amekiri haitokuwa mechi ya kitoto kutokana na Yanga kupoteza mechi yake iliyopita.

"Tuko vizuri, na tuko tayari kucheza na Yanga, tunajua mechi itakuwa ngumu kwa sababu hawakufanya vizuri mechi iliyopita, hivyo wataingia kwa nguvu sana tunalijua hilo, ndiyo maana pamoja na ufundi tunajaribu kuwatengeneza wachezaji wetu kisaikolojia. Tunawaheshimu Yanga kwa sababu kwa miaka miwili au mitatu wamekuwa na kikosi kizuri, lakini sisi pia tuko imara," alisema Moroco.


SUPA JACKPOT

MECHI WIKI HII

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 07/10/23 | 19:30 | Mallorca vs Valencia | 2.45 | 3.05 | 2.90 |
| 02. 07/10/23 | 19:30 | Werder Bremen vs Hoffenheim | 2.70 | 3.65 | 2.29 |
| 03. 07/10/23 | 22:00 | Reims vs Monaco | 2.60 | 3.55 | 2.42 |
| 04. 08/10/23 | 15:15 | FC Lugano vs Servette Geneva | 2.12 | 3.45 | 2.80 |
| 05. 08/10/23 | 16:00 | Frosinone vs Verona | 2.26 | 3.30 | 3.00 |
| 06. 08/10/23 | 16:00 | Lazio vs Atalanta | 2.55 | 3.25 | 2.60 |
| 07. 08/10/23 | 16:00 | Tanzania Prisons vs Mtibwa Sugar | 2.25 | 2.80 | 3.40 |
| 08. 08/10/23 | 16:00 | GIF Sundsvall vs IK Brage | 2.48 | 3.20 | 2.48 |
| 09. 08/10/23 | 16:00 | Brighton vs Liverpool | 2.80 | 3.80 | 2.18 |
| 10. 08/10/23 | 16:00 | Wolverhampton vs Aston Villa | 3.30 | 3.40 | 2.07 |
| 11. 08/10/23 | 16:00 | West Ham vs Newcastle | 3.00 | 3.55 | 2.14 |
| 12. 08/10/23 | 17:30 | Lausanne-Sport vs FC Luzern | 2.44 | 3.35 | 2.42 |
| 13. 08/10/23 | 17:30 | Famalicao vs Vitoria Guimaraes | 2.55 | 3.15 | 2.70 |
| 14. 08/10/23 | 18:05 | Lens vs Lille | 2.15 | 3.45 | 3.05 |
| 15. 08/10/23 | 18:30 | Arsenal vs Manchester City | 2.70 | 3.35 | 2.43 |
| 16. 08/10/23 | 18:30 | Hammarby vs Hacken | 2.35 | 3.35 | 2.50 |
| 17. 08/10/23 | 19:30 | Alaves vs Betis | 2.75 | 3.10 | 2.55 |

MECHI ZA USHINDI

"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMAMOSI - 07/10/2023

| MUDA | GAME ID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 14:30 | 4555 | Luton Town vs Tottenham | 6.19 | 4.75 | 1.48 |
| 15:00 | 1406 | Nairobi City Stars FC vs Kenya Police | 4.08 | 3.15 | 1.87 |
| 15:00 | 1645 | Muranga Seal vs Sofapaka | 2.27 | 3.31 | 2.79 |
| 15:00 | 2557 | Cadiz CF vs Girona | 3.19 | 3.39 | 2.26 |
| 15:00 | 3910 | Hawassa Kenema SC vs Fasil Kenema | 2.90 | 2.95 | 2.41 |
| 15:00 | 5554 | Ulinzi Stars vs Kariobangi Sharks | 2.56 | 2.92 | 2.72 |
| 16:00 | 1045 | Nkwazi vs Zanaco | 2.19 | 2.65 | 3.50 |
| 16:00 | 1686 | AFC Leopards vs Gor Mahia | 3.52 | 2.92 | 2.11 |
| 16:00 | 1874 | Mufulira Wanderers vs Nkana FC | 2.41 | 2.65 | 3.05 |
| 16:00 | 1927 | Inter vs Bologna | 1.41 | 4.94 | 7.21 |
| 16:00 | 2807 | Zesco United vs Green Buffaloes | 1.75 | 3.06 | 4.72 |
| 16:00 | 3279 | Geita Gold FC vs Young Africans | 6.90 | 4.34 | 1.40 |
| 16:00 | 3378 | El Daklyeh vs Al Masry Club | 4.09 | 3.14 | 1.92 |
| 16:00 | 3957 | Prison Leopards vs Red Arrows | 2.97 | 2.67 | 2.51 |
| 16:00 | 4312 | Ankaragucu vs Kayserispor | 2.11 | 3.36 | 3.20 |
| 16:00 | 4645 | KMC vs Ihefu FC | 2.15 | 3.02 | 3.41 |
| 16:30 | 3338 | RB Leipzig vs VfL Bochum | 1.25 | 6.57 | 10.06 |
| 16:30 | 3377 | Borussia Dortmund vs Union Berlin | 1.62 | 4.22 | 5.15 |
| 16:30 | 4269 | Augsburg vs SV Darmstadt | 1.89 | 3.76 | 3.91 |
| 16:30 | 5714 | Stuttgart vs VfL Wolfsburg | 2.03 | 3.70 | 3.50 |
| 17:00 | 2014 | Manchester Utd vs Brentford | 1.69 | 4.11 | 4.62 |
| 17:00 | 2888 | Burnley vs Chelsea | 4.62 | 3.95 | 1.72 |
| 17:00 | 3173 | Everton vs Bournemouth | 1.96 | 3.65 | 3.75 |
| 17:00 | 3196 | Fulham vs Sheffield Utd | 1.64 | 3.85 | 5.54 |
| 17:00 | 3289 | AS Slimane vs Africain | 4.84 | 3.13 | 1.71 |
| 17:00 | 3841 | Stade Tunisien vs ES Sahel | 3.55 | 3.00 | 1.99 |
| 17:15 | 2518 | Real Madrid vs Osasuna | 1.32 | 5.55 | 9.05 |
| 17:30 | 4205 | GD Chaves vs Gil Vicente | 2.43 | 3.33 | 2.68 |
| 17:30 | 5777 | Sporting Farense vs FC Vizela | 2.09 | 3.33 | 3.28 |
| 17:45 | 3730 | Ben Aknoun vs US Souf | 1.97 | 3.06 | 3.77 |
| 17:45 | 3838 | CR Belouizdad vs USM Khenchela | 1.39 | 4.07 | 7.54 |
| 18:00 | 4132 | Metz vs Nice | 4.62 | 3.75 | 1.77 |
| 18:00 | 5622 | Union Touarga vs FAR Rabat | 4.84 | 3.48 | 1.62 |
| 19:00 | 1631 | Basaksehir vs Gaziantep BB | 1.80 | 3.47 | 4.14 |
| 19:00 | 2001 | Juventus vs Torino | 1.90 | 3.35 | 4.44 |
| 19:00 | 2580 | Orlando Pirates vs Mamelodi Sundowns | 2.98 | 2.98 | 2.28 |
| 19:00 | 3398 | Antalyaspor vs Galatasaray | 4.73 | 3.70 | 1.66 |
| 19:00 | 4653 | National Bank vs Zamalek | 4.09 | 3.14 | 1.92 |
| 19:00 | 5052 | Talaea El Gaish vs Coca Cola | 3.23 | 2.74 | 2.44 |
| 19:30 | 3422 | Crystal Palace vs Nottingham | 2.24 | 3.19 | 3.45 |
| 19:30 | 4185 | Mallorca vs Valencia | 2.44 | 3.07 | 3.18 |
| 19:30 | 5221 | Werder Bremen vs Hoffenheim | 2.73 | 3.81 | 2.38 |
| 20:00 | 5084 | Sporting Braga vs Rio Ave | 1.31 | 4.99 | 8.38 |
| 21:00 | 1610 | JS Kabylie vs USM Alger | 1.62 | 3.41 | 5.29 |
| 21:45 | 2239 | Genoa vs AC Milan | 3.84 | 3.48 | 1.99 |
| 22:00 | 1747 | Reims vs Monaco | 2.68 | 3.66 | 2.48 |
| 22:00 | 4691 | Sevilla FC vs Rayo Vallecano | 1.88 | 3.56 | 4.23 |
| 22:00 | 5703 | Vitesse Arnhem vs SBV Excelsior | 1.67 | 3.96 | 4.16 |
| 22:30 | 3724 | GD Estoril vs Benfica | 8.94 | 5.76 | 1.25 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# Michezo

Jumamosi Oktoba 7, 2023

Nipashe




Messi kurudi Barcelona

UK. 21




Gamondi

Robertinho

# Simba yapewa tena Wydad, Yanga SC yaangukia Al Ahly

## ●●● Ni hatua ya makundi Ligi ya Mabingwa Afrika,mechi za kwanza kuchezwa...

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI Simba ikipangwa Kundi B na timu za Wydad Casablanca ya Morocco, ASEC Mimosas ya Ivory Coast na Jwaneng Galax ya Botswana, Yanga wameangukia kwa Mabingwa watetezi Ligi ya Mabingwa Afrika, Al Ahly ya Misri katika kundi D wakiwa pamoja na timu za CR Belouizdad ya Algeria na Medeama FC ya Ghana.

Simba ambao katika kundi lao itakutana na timu zote tatu ambazo imewahi kucheza nazo katika vipindi tofauti miaka ya hivi karibuni, itaanzia nyumbani mechi yake ya kwanza dhidi ya ASEC kati ya Novemba 24 na 25, wakati Yanga itakuwa ugenini nchini Algeria kucheza na CR Belouizdad kati ya tarehe hizo.

Kwa mujibu wa ratiba iliyopangwa jana jioni nchini Afrika Kusini, haikuwa kama wengi walivyotarajia kuwa timu za Simba na Yanga ambao ni watani wa jadi wangeweza kupangwa kundi moja, badala yake 'zimekwepana' huku timu za nchini Tunisia, Etoile du Sahel na Esperance zikijikuta kwenye kundi moja ambalo ni Kundi C.

Yanga ambayo imetinga makundi kwa mara ya kwanza baada ya miaka 25, itakutana tena na Medeama FC ambao wamewahi kucheza nao kwenye hatua ya makundi ya Kombe la Shirikisho Afrika mwaka 2016 huku Yanga ikimaliza nyuma ya timu hiyo.

Yanga pia ilikutana na Al Ahly mwaka huo kwenye hatua ya pili ya Ligi ya Mabingwa Afrika na kutolewa, ndipo ilipoangukia kombe la Shirikisho na kufanikiwa kutinga hatua ya makundi.

**Kwenye Kundi hilo pia Yanga itakuwa na timu ambayo hai jawahi kucheza nayo, CR Bel ouizdad ya Algeria.**

Simba itapata nafasi ya kulipiza kisasi mbele ya Wydad Casablanca waliowaondoa kwenye hatua ya robo fainali msimu uliopita.

Katika hatua hiyo, mchezo wa kwanza Simba ilishinda bao 1-0 kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, na kukubali kipigo kama hicho kwenye mchezo wa marudiano uliochezwa Aprili 23 kabla ya kutolewa kwa mikwaju ya penalti 4-3.

Simba pia ilikuwa kundi moja na Asec Mimosas mwaka jana kila timu ikishinda nyumbani kwake, Simba ikishinda 3-1 nyumbani, lakini ikachapwa mabao 3-0 ugenini. Ipo pia timu maarufu nchini Jwaneng Galaxy ya Botwana ambayo iliitoa Simba kwenye Ligi ya Mabingwa Afrika, 2021 kwenye Uwanja wa Benjamini Mkapa na kuifanya kuangukia Kombe la Shirikisho ilikokwenda kukutana na Asec Mimosas.

Katika mechi ya kwanza ugenini, Simba iliifunga Jwaneng Galaxy mabao 2-0, lakini ikajikuta ikipachikwa mabao 3-1 nyumbani, ikatoka kwa bao la ugenini matokeo ya jumla yakiwa mabao 3-3.

Mamelodi Sundowns ya Afrika Kusini ipo kwenye Kundi A linalotajwa kuwa kundi la kifo ikipangwa na Pyramids ya Misri, TP Mazembe ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo pamoja na FC Nouadhibou ya Mauritania.

Ndugu wawili, Esperance na Etoile du Sahel za Tunisia zipo Kundi C na Al Hilal ya Sudan na Petro de Luanda ya Angola.

Kwa mujibu wa ratiba hiyo baada ya mechi za kwanza, Yanga itarudi nyumbani kucheza mechi yake ya pili dhidi ya Al Ahly kati ya Desemba 1 na 2 wakati tarehe hizo hizo, Simba itakuwa ugenini Botswana kucheza na Jwaneng Galaxy.

# Yanga SC kumaliza hasira kwa Geita Gold

**Na Adam Fungamwango**

HASIRA za Yanga za kufungwa mabao 2-1 katika mchezo wao uliopita dhidi ya Ihefu FC wamepania kuzimaliza leo mbele ya Geita Gold FC wanaocheza nao kwenye Uwanja wa CCM Kirumba jijini Mwanza.

Kocha wa mabingwa hao watetezi, Miguel Gamondi, aliiambia Nipashe jana kuwa hawatofanya makosa tena ya kupoteza mchezo kama ilivyotokea Mbarali.

Miguel, alisema anafahamu nini walikosea na kupelekea kupoteza mchezo huo na leo amepania kufuta makosa waliyoyafanya.

" Hatutarudia makosa, muda mwingine mpira wa miguu una matokeo ya kushangaza, tumejiandaa na tupo tayari kurudisha furaha ya mashabiki wetu," alisema Gamondi na kuongeza,

"Tunataka kufanya vizuri kwa sababu kama kocha unaifundisha Yanga unahitajika kushinda mechi, tutafanya kila tunachoweza kurudisha furaha kwa mashabiki kwa kupata ushindi na kufuta makosa ya kwenye mchezo uliopita, nina imani na wachezaji wangu," alisema.

Kocha huyo ana zaidi ya miaka 25 amekuwa akifundisha soka kwenye nchi mbalimbali, lakini kwa sasa ameanza kujifunza soka la Tanzania.

"Nina zaidi ya miaka 25 ya kufundisha soka hapa Afrika katika nchi mbalimbali, uzoefu hauwezi kujifunza kwenye chuo chochote kile, lakini sasa nimeanza kuifahamu ligi ya Tanzania na napenda kujifunza, na tukifanya makosa ndiyo tunajifunza.

Nataka pia nisema baadhi ya viwanja haviwezi kukupa uhuru wa kucheza soka safi badala yake unatakiwa upige mbele na kukimbizana wakati si falsafa yangu, pia naomba waamuzi wazilinde timu zinazotaka kucheza soka dhidi ya zile ambazo zinapoteza muda," alisema Gamondi.

Aidha, aliwageukia mashabiki akisema kuna wakati wanaona kama vitu ni rahisi, lakini ukweli ni kwamba wachezaji pia ni binadamu wanaoweza kufanya makosa kama mtu yeyote yule.

"Kuna wakati mashabiki na watu wengine wanaona ni rahisi, lakini kwa sisi makocha na wachezaji tuna kazi ngumu, angalia hatuna muda wa kumpumzika,

INAENDELEA UK 23

9 770856 541002 >

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042